epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Alhamisi Juni 6, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581699
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital




UKURASA 22

**'KUNA WATU WALININYIMA FURAHA PSG'**

# Lori laua watu 13 kwenye mteremko

UKURASA 2



UKURASA WA 22

## FEDHA KUMPELEKA DE BRUYNE SAUDIA

KELVIN De Bruyne amesema yuko "wazi" kuhamia Ligi Kuu ya Saudia Arabia kutokana na faida...

## Samia: Shida kuu ya bajeti zetu Waafrika ni vipaumbele

UKURASA 3



Baadhi ya wananchi wakishirikiana na Askari Polisi kuondoa moja ya pikipiki ambazo zilihusika kwenye ajali ya lori lililosababisha vifo vya watu 13 majeruhi 18 katika mteremko wa Simike jijini Mbeya jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

UKURASA WA 5

## BoT YAONYA KUUNDA PAMBO LA NOTI, ADHABU NI KWENDA JELA

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT) imeonya watu ambao...



UKURASA WA 4

## PROF. MKENDA ASEMA 'BOOM' LILILOTOWEKA MIEZI 6, LIMERUDI

SERIKALI imeanza kutekeleza kwa vitendo agizo la Katibu...




UKURASA WA 19

## MAKONDA ATUMIA WARAKA WA CAG KUPEKUA KASHFA KILA H/SHAURI

BAADA ya ziara ya siku sita katika wilaya zote za mkoa, Mkuu wa...



MWENYEKITI WA BODI YA WAKURUGENZI WA SPORTPESA, TARIMBA ABBAS, AKIKABIDHI MFANO WA HUNDI YA SHILINGI MILIONI 537.5 KWA RAIS WA KLABU YA YANGA, MHANDISI HERSI SAID KAMA BONASI YA KUFANYA VIZURI KWENYE MSIMU WA 2023/24 KATIKA MASHINDANO YA LIGI YA MABINGWA AFRIKA (CAF), KUTWAA MAKOMBE YA LIGI KUU TANZANIA BARA NA LIGI YA SHIRIKISHO TANZANIA.





## Msigwa aibukia mkutano wa Lissu

UKURASA 19

**MICHEZO** **SPORTPESA YAIPA YANGA MAMILIONI** UK.24

**KATUNI** UK.6



Rais Samia Suluhu Hassan akiteta jambo na Rais wa Zimbabwe, Emmerson Mnangagwa wakati wa mkutano wa biashara kati ya Korea na Afrika, jijini Seoul, Jamhuri ya Korea jana. **PICHA: IKULU**

# Lori laua watu 13 kwenye mteremko

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATU 13 wamefariki dunia papohapo na wengine 18 kujeruhiwa katika ajali ya barabarani iliyotokea jana kwenye mteremko wa Mbembela, jijini Mbeya.

Ni baada ya lori lililokuwa limebeba kokoto kufeli breki na kuparamia magari mawili, pikipiki na guta.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi Benjamin Kuzaga, akiwa eneo la tukio, alitaja lori lililosababisha ajali hiyo ni aina ya Scania lenye namba za usajili T. 979 CVV na tela lenye namba za usajili T. 758 BEU ambalo lilikuwa linatoka Uyole kuelekea Barabara ya Tunduma.

Alisema lori hilo liligonga gari dogo aina ya Harrier lenye namba za usajili T. 120 DEL na kupoteza mwelekeo kisha kugonga gari aina ya Coaster lenye namba za usajili T. 167 DLF lililokuwa linatokea Tunduma kwenda jijini Mbeya.

Alisema lori hilo liliparamia waendesha pikipiki, maarufu bodaboda, na guta ambalo lilikuwa limebeba mahindi.

Alisema vifo na majeruhi wengi ni waliokuwa katika gari la abiria ambalo liliburuzwa mpaka kwenye mtaro. Wengi wao walikuwa wamebanwa.

"Dereva wa lori tumempata na tunaendelea kufuatilia hawa wa vyombo vingine ili kubaini kama ni miongoni mwa majeruhi ama waliopoteza maisha, lile gari dogo aina ya Harrier kilichotokea ni uharibifu wa chombo," alisema Kuzaga.

Baadhi ya wananchi walioshuhudia ajali hiyo walisema waliona gari hilo likiwa linashuka mlima huo likiwa limewasha taa na kupiga honi kuashiria hatari.

Mmoja wa mashuhuda hao, Bashiri Mwaluwanda alisema dereva wa lori hilo alifanikiwa kuyakwepa baadhi ya magari na bajaji kwenye mteremko huo na baada ya kugonga gari dogo, alipoteza mwelekeo na kuanza kuyumba.

Alisema kuwa baada ya kugonga basi dogo la abiria (coaster) na kuanguka walianza kuokoa baadhi ya waathirika hasa majeruhi na kuwakimbiza hospitalini kwa kutumia pikipiki na bajaji kabla ya magari ya kubeba wagonjwa kufika eneo la tukio.

Alisema kuwa baadhi ya watu ambao walikuwa wamebanwa kwenye basi dogo la abiria waliondolewa baada ya askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kufika na vifaa.

"Watu waliofariki (dunia) ni wengi, dereva wa lori amejitahidi sana kuyakwepa magari mengine na yaliyokuwa yanapandisha kwenye huu mteremko, yule wa coaster alishindwa kumkwepa kwa sababu ni eneo la matuta," alidai Mwaluwanda.

Mapinduzi Mwambambe, shuhuda mwingine wa ajali hiyo, alisema alipigiwa simu na mdogo wake ambaye anafanya shughuli zake eneo la Simike, akamweleza kwamba kuna lori limefeli breki linashuka uelekeo wa Mbembela na akamtahadharisha kama alikuwa barabarani, alipaswa kuondoka.

Alisema kabla mdogo wake hajamaliza kutoa maelezo hayo, alisikia kishindo barabarani na alipokwenda kuangalia akakuta lori hilo limeshagonga gari la abiria ndipo akaanza kushiriki uokoaji.

Alisema uokoaji ulikuwa rahisi kwa sababu ni eneo la jeshini na hivyo askari wengi wa kikosi cha Jeshi cha 844 Itende KJ walishiriki uokoaji pamoja na kutoa taarifa kwa vyombo vingine vya dola.

Nipashe lilishuhudia magari manne ya kubeba wagonjwa, mawili ya Jeshi la Polisi na moja la Jeshi la Wananchi (JWTZ) yakisomba majeruhi na miili ya marehemu kupeleka katika Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya.

## Dk. Mpango asisitiza mambo matatu uhifadhi mazingira

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MAKAMU wa Rais Dk. Philip Mpango, amesisitiza mambo matatu yatakayosaidia kufanikisha juhudi za kuhuisha ardhi iliyoharibiwa, kujenga ustahimilivu dhidi ya ukame na kuzuia kuenea kwa jangwa nchini.

Mambo hayo ni pamoja na taifa kuimarisha menejimenti ya usimamizi wa mazingira ikiwamo kubadili mfumo wa ufugaji.

Dk. Mpango alibainisha hayo jana wakati akifunga maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani iliyofanyika kitaifa jijini Dodoma.

"Tunahitaji wafugaji wetu waanze kufuga kisasa kwenye mashamba yao ya mifugo na kudhibiti idadi kubwa ya mifugo inayozidi uwezo wa upatikanaji wa malisho.

"Ni lazima kubadili kilimo ili kiwe endelevu na cha kisasa zaidi, kinachozingatia matumizi ya mboji na marejea, matumizi ya matandazo ya majani ili kuhifadhi unyevu, matumizi ya teknolojia za kijani na kudhibiti uchomaji ovyo wa misitu na vichaka," alisema.

"Pili kifungu cha 89 cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) Sura ya 288, kinazipa Halmashauri mamlaka ya kutunga sheria ndogo za utunzaji wa mazingira na udhibiti wa taka. Licha ya kuwapo kwa sheria ndogo zilizotungwa kukabiliana na changamoto hiyo na kuhakikisha miji yetu inakuwa safi, bado taka za aina mbalimbali zinazagaa ovyo mitaani," aliongeza.

Dk. Mpango alisema kutokana na hali hiyo viongozi wa serikali, bunge, chama, dini na asasi za kiraia, waungane kupaza sauti ili kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kutunza mazingira.

"Aidha, naziagiza halmashauri zote kusimamia ipasavyo utekelezaji wa sheria ndogo za kulinda mazingira na kuhakikisha hatua za kisheria zinachukuliwa dhidi ya wanaokwenda kinyume," alisisitiza.

Kadhalika, alisema kila mwananchi awe mlinzi wa mwenzake katika kuhakikisha hakuna mwananchi anayetupa taka hovyo na kuchafua mazingira yetu.

Hata hivyo, alisema taka ni mali pale zinapobadilishwa na kuwa malighafi ya viwanda.

"Ninazihimiza halmashauri zote zifanye jitihada kuhamasisha na kuvutia viwanda vyenye teknolojia ya kubadili taka za aina mbalimbali ili ziweze kutumika tena kama bidhaa. Pia, natoa wito kwa wananchi na sekta binafsi kuchangamkia fursa zilizopo katika ukusanyaji na urejelezaji wa taka," alisema.

## HABARI KITAIFA

# Sheria ya Usalama Barabarani kufumuliwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imeweka mikakati madhubuti itakayosaidia kukomesha ajali za barabarani ikiwamo kuifanyia marekebisho Sheria ya Usalama Barabarani na muswada wa sheria umeshawasilishwa bungeni na kusomwa kwa mara ya kwanza.

Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Jumanne Sagini, alisema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum, Felista Njau (CCM), kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

Katika swali lake la msingi, mbunge huyo alitaka kujua serikali ina mkakati gani madhubuti wa kukomesha kabisa ajali za barabarani ambazo zimekuwa zikigharimu maisha ya watu wengi.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Sagini alisema serikali imeweka mikakati madhubuti itakayosaidia kukomesha ajali za barabarani ambayo inahusisha kuifanyia marekebisho Sheria ya Usalama Barabarani.

Sagini alisema mkakati mwingine ni kuboresha miundombinu ya barabara na kuweka alama za matumizi ya barabara, kuandaa utaratibu wa kufunga mifumo ya TEHAMA barabarani ili kufuatilia na kudhibiti ajali.

"Pia kuandaa utaratibu wa ukaguzi wa lazima wa vyombo vya moto ili kudhibiti ubora wa vyombo hivyo viwapo barabarani na kuendelea kutoa elimu ya usalama barabarani kupitia vituo vya runinga na redio, elimu kwenye shule za msingi, sekondari na vyuo, vituo vya mabasi, vituo vya bodaboda na bajaji, vituo vya ukaguzi wa magari, shule za udereva na kutoa mafunzo kwa madereva wa serikali, taasisi za umma na watu binafsi," alisema.

# Samia ataja vikwazo utekelezaji wa bajeti katika nchi za Afrika

**Na Salome Kitomari,** KOREA

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema utekelezaji wa bajeti za Afrika unakabiliwa na changamoto ya vipaumbele vinavyoshindana ikiwamo utoaji huduma za kijamii, jambo linalofanya isitosheleze.

Akizungumza jana kwenye Jukwaa la Miundombinu kati ya Korea na Afrika lililofanyika jijini Seoul, Korea Kusini, Rais Samia alisema bajeti ya miundombinu Afrika kwa mwaka ni takribani dola bilioni 170 lakini kiasi kinachopatikana ni dola bilioni 62.

Alisema Afrika ina nakisi ya bajeti ya miundombinu ya dola za Marekani bilioni 108 kwa mwaka licha ya kwamba miundombinu ndiyo moyo wa uchumi.

Rais Samia pia aliendelea kuikaribisha Korea Kusini ambayo ni nchi ya 12 kwa uchumi mkubwa duniani na sekta binafsi, kuongeza uwekezaji katika ujenzi wa miundombinu hasa reli, gesi na miundombinu ya kijiditali.

Awali, akifungua mkutano huo, Waziri wa Ardhi, Miundombinu na Uchukuzi wa Korea, Sang-Woods Park, alisema kuna uwezekano mkubwa wa kuwekeza Afrika kutokana na kuwa bara la pili kwa ukubwa lenye zaidi ya watu bilioni 1.3 na rasilimali nyingi.

Wakati huo huo, Tanzania na Korea zimetia saini mkataba wa dola milioni 163.6 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Rufani Binguni na Chuo cha Mafunzo ya Afya visiwani Zanzibar.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kutiwa saini kwa mkataba huo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Zanzibar, Dk. Saada Mkuya Salum, alisema miradi hiyo inatakiwa kutekelezwa ndani ya miaka mitano lakini serikali itahakikisha inakamilika mapema.



"Mradi huu umepatikana kutokana na ushirikiano uliopo baina ya Korea na Tanzania na fedha zimepitia Benki ya Exim Korea. Mradi huu utaimarisha sekta ya afya Zanzibar na kujenga wodi za watoto, wanawake na magonjwa ya moyo.

"Kituo cha elimu ya afya kitafundisha madaktari wa aina mbalimbali watakaobobea kwenye kutibu magonjwa mbalimbali. Itakuwa hospitali ya aina yake kwa kuwa itakuwa na vifaa vya kisasa vya matibabu na utaalamu na matumizi ya teknolojia ya kisasa," alisema.

Waziri Mkuya alisema Zanzibar ilisubiri kwa hamu utekelezaji wa mradi huo na sasa fedha za utekelezaji zimepatikana.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Exim Korea, Hwang Kiyeon, alisema hospitali hiyo itakuwa vifaa vya teknolojia ya kisasa kwa ajili ya kuboresha sekta ya afya Tanzania.

Alisema ushirikiano kati ya Korea na Tanzania utaendelea kuimarika huku Tanzania ikiwa na nafasi ya pekee kutokana na hatua zilizochukuliwa za kushirikiana wakati wa mkutano wa Korea Afrika uliofanyika juzi na jana.

Rais Samia anahitimisha ziara yake nchini Korea kwa kuzungumza na Watanzania wanaoishi nchini hapa.


## Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya **epaper.ippmedia.com** utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza **"subscribe"**
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa **kadi ya benki** malipo kwa **mtandao wa simu** unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa **namba ya simu** unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. **Kwa benki** unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

6. Unafungua website yako ya **www.ippmedia.com** upande wa kulia utaona **"E-Paper"** utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

# Prof. Mkenda asema 'boom' lililotoweka miezi 6 limerudi

**Na Romana Mallya,**

SERIKALI imeanza kutekeleza kwa vitendo agizo la Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, kuhusu ulipaji wa fedha za kujikimu (boom) kwa wanafunzi wa vyuo vikuu ambao baadhi wamesema hawajalipwa miezi sita.

Juzi, katika mkutano wa hadhara uliofanyika wilayani Arumeru mkoani Arusha, Balozi Nchimbi baada ya kupokea malalamiko ya wanafunzi kuhusu posho hizo za kujikimu, alitoa siku 27 kwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, kumaliza tatizo hilo.

Mwanafunzi wa Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru, Arusha, Digna Nasari, ambaye ni Katibu Mwenezi wa CCM Kata ya Ambureni, alimweleza Katibu Mkuu huyo kuwa mpaka sasa ni miezi sita wanachuo chuoni hapo hawajapata fedha. Taarifa kutoka kwa mwanafunzi huyo zinaeleza kuwa baada ya maelekezo ya Katibu Mkuu fedha zimeanza kuingizwa katika kaunti za wanafunzi kuanzia jana jioni.

Awali jana, Prof. Mkenda ambaye ni Mbunge wa Rombo alisema kwenye kikao cha ndani cha viongozi na mabalozi wa CCM mkoani Kilimanjaro mbele ya Katibu Mkuu CCM kuwa wizara imepokea maelekezo hayo.

“Ndugu Katibu Mkuu, jana pale Arusha ulitoa maelekezo kuhusu suala la ‘boom’ na ninaomba nitumie nafasi hii kusema suala hilo tutalifanyia kazi na kabla ya muda uliyotoa wanafunzi wote nchini watalipwa,” alisema.

Juzi, Balozi Nchimbi alisema: "Leo ni tarehe nne litakwisha mwisho wa mwezi huu. Kuna mtu mmoja kasema mwisho wa mwezi huu ni mbali sana lakini ninataka niwaambie kama wamesubiri miezi sita, wanaweza kusubiri siku hizo chache.

“Lakini lazima tatizo liishe na liwe na utatuzi wa kudumu. Tunapotoka hapa kiongozi wenu atupatie namba ya simu ili tulifuatilie kwa karibu awe anatupa habari wasije kutuambia wameshalipa kumbe bado hawajalipa.”







Mhariri Mtendaji wa Gazeti la The Guardian, Wallace Mauggo, akimlisha keki Mhariri Mtendaji wa Gazeti la Nipashe, Beatrice Bandawe, katika chumba cha habari cha Kampuni ya The Guardian Ltd (TGL), Mikocheni Dar es Salaam jana, kama ishara ya kumpongeza baada ya kupata Tuzo ya Mwanamke Kiongozi katika Chombo cha Habari 2024, iliyotolewa na Umoja wa Wachapishaji wa Magazeti Duniani (WAN-IFRA), hivi karibuni. **PICHA: JOHN BADI**

# Jela miaka saba kumtapeli waziri

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, imemhukumu Innocent Chengula kifungo cha miaka saba jela baada ya kupatikana na hatia ya kumtapeli Sh. milioni nne Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwani Kikwete.

Sambamba na kifungo hicho, mahakama imemwamuru Chengula kumlipa mlalamikaji (Ridhiwani) fedha hizo. Pia mahakama imeamuru simu na laini alizokutwa nazo zitaifishwe kuwa mali ya serikali.

Chengula alimtapeli Ridhiwani baada ya kujitambulisha kwake kuwa yeye ni Dk. Hassan Abbas, wakati akijua si kweli.

Hukumu hiyo ilitolewa juzi na Hakimu Mkazi Mkuu wa Mahakama hiyo, Yusto Ruboroga, baada ya kusikiliza mashahidi 14 wa upande wa mashtaka, vielelezo na sheria zinazohusiana na mashtaka hayo.

Akisoma hukumu hiyo, Hakimu Ruboroga alisema mashahidi hao wamethibitisha mashtaka hayo bila kuacha shaka yoyote.

Alisema katika shtaka la kwanza ambalo ni kutumia ujumbe kwa mtandao wa kijamii wa WhatsApp akijitambulisha kwa Ridhiwani Kikwete na Wallece Karia (Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania- TFF) kuwa yeye ni Dk. Hassan Abbas, alimhukumu kulipa faini ya Sh. milioni 12 au kwenda jela miaka saba.

Katika shtaka la pili ambalo alijitambulisha kwa Karia kuwa yeye ni Dk. Hassan Abbas, alimhukumu kulipa faini ya Sh. milioni 12 au jela miaka saba na shtaka la tatu ambalo ni kujipatia Sh. milioni nne kwa njia ya udanganyifu, alihukumiwa kifungo cha miaka saba jela.

Pia alisema katika shtaka la nne hadi la sita ambalo ni kutumia laini ambayo imesajiliwa kwa majina ya watu wengine, alihukumiwa kila shtaka kulipa faini ya Sh. milioni tano au jela miezi sita na adhabu hiyo inakwenda kwa pamoja.

"Mahakama inakuhukumu mshtakiwa kifungo cha miaka saba jela na adhabu ya mashtaka hayo yanakwenda kwa pamoja. Kwa hiyo utatumikia kifungo gerezani miaka saba tu," alisema Hakimu Ruboroga.

Kabla ya kutolewa kwa hukumu hiyo, Wakili wa Serikali, Glory Kilawa, aliomba mahakama kutoa adhabu kali kwa mshtakiwa ili iwe fundisho kwake na wengine wenye tabia hizo za kuwaibia watu mtandaoni.

Baada ya mshtakiwa kupewa nafasi ya mahakama, aliomba mahakama impunguzie adhabu kwa kuwa amekaa gerezani mwaka mmoja na miezi minane.

Hakimu Ruboroga alisema mahakama inampa adhabu kali mshtakiwa ili iwe fundisho kwa wengine ambao wanaiba fedha za watu mtandaoni wakiwasumbua raia.

Kwa mujibu wa hati ya mashtaka, kati ya Julai 8, 2022 eneo lisilofahamika ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mshtakiwa alitumia ujumbe katika mtandao wa kijamii wa WhatsApp akijitambulisha kwa Ridhiwani Kikwete kuwa yeye ni Dk. Abbas.

Katika shtaka la pili, siku hiyo alijitambulisha kwa Wallace Karia kuwa yeye ni Dk. Abbas

Katika shtaka la tatu ambalo ni kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu, mshtakiwa alitenda kosa hilo Julai 26, 2022 ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alijipatia Sh. milioni nne kutoka kwa Ridhiwan baada ya kujifanya ni Dk. Abbas.

Shtaka la nne hadi sita, la kutumia laini iliyosajiliwa kwa majina ya Nuru Maulid, Deogratius Kimario na Asha Mkai, bila kutoa taarifa kwa mtoa huduma, alitenda kosa hilo Juni na Agosti, 2022.

# Kilichompeleka DC Baraza la Maadili

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Tanganyika mkoani Katavi, Onesmo Buswelu, juzi alifikishwa mbele ya Baraza la Maadili kwa tuhuma za ukiukwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

Sababu kubwa ya kufikishwa katika baraza hilo ni tuhuma za makosa mawili ambayo ni matumizi ya lugha chafu dhidi ya watumishi wa umma na kukamata watu na kuwaweka mahabusu kinyume cha sheria. Aidha, mkuu huyo wa wilaya, alitoa machozi wakati akijitetea baada ya kusomewa tuhuma zinazomkabili.

Kikao cha kusikiliza tuhuma dhidi ya kiongozi huyo kilifanyika jijini hapa katika ukumbi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa chini ya Mwenyekiti wa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Jaji Mstaafu Rose Teemba na mjumbe wa baraza hilo, Peter Ilomo.

Wakili wa Serikali, Hassan Mayunga, aliliambia baraza kuwa mlalamikiwa wakati akitekeleza majukumu yake ya kikazi, amekuwa akitumia lugha chafu na matusi kwa watumishi na watendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika kinyume cha kifungu cha 6(1)(a) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

"Mheshimiwa Mwenyekiti, mlalamikiwa wakati akitekeleza majukumu yake ya kikazi, amekuwa akiwakamata na kuwaweka mahabusu wananchi, watumishi wa umma na watendaji wa serikali katika Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika kinyume cha kifungu cha 6(1) (c) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

"Kushindwa kutimiza wajibu huo wa kisheria ni ukiukwaji wa maadili ya viongozii wa umma kwa mujibu wa kifungu cha 6 (2) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma," alisema

upande wa mlalamikaji uliwapeleka mashahidi watatu ambao ni Leonard Kansimba, Ofisa Uchunguzi wa Sekretarieti ya Maadili na Raymond Bernard ambaye Mkuu wa Shule ya Sekondari Kakoso wilayani Tanganyika anayedai kutolewa lugha ya matusi na kiongozi huyo.

Shahidi mwingine ni Primo Kampamba, fundi ujenzi kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika aliyelieleza Baraza kuwa mkuu huyo wa wilaya alimweka mahabusu bila kufuata taratibu.

Mlalamikiwa aliyakana mashtaka yote mawili na kudai mbele ya baraza kuwa tuhuma zote ni za kutengeneza. Alisema amekuwa akisimamia vizuri utekelezaji wa miradi ya maendeleo wilayani humo kwa kuhakikisha fedha za miradi zinatumika ipasavyo bila ubadhirifu wa aina yoyote.

"Katika kutenda kwangu kazi kama mkuu wa wilaya ya Tanganyika, sijatumia lugha chafu na za matusi kwa watumishi na watendaji wa wilaya. Kazi hizi za ukaguzi wa miradi sijazifanya peke yangu, nilikuwa na viongozi wengine wa kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya.

"Kwa ukaribu na udhibiti huo, imesababisha wanaodhibitiwa kutofurahi," aliliambia baraza huku akitokwa na machozi.

Baada ya kusikiliza pande zote mbili, mwenyekiti alimweleza mlalamikiwa kuwa kazi iliyobaki sasa ni baraza kufanya upekuzi na tathmini na kama kutakuwa na chochote mamlaka zitamjulisha.

## BoT yaonya kuunda pambo la noti, adhabu jela

**Na Ashton Balaigwa,** DODOMA

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT) imeonya watu ambao wamekuwa na tabia ya kuhifadhi fedha kwenye maziwa, soksi, chini ya magunia na kufunga fundo kwenye kanga, ikisisitiza kunafedhehesha fedha ya Tanzania.

Pia imepiga marufuku fedha kuhifadhiwa sehemu za siri pamoja na kutengenezwa mataji kwenye sherehe, atakayebainika atachukuliwa hatua za kisheria kwa kuwa vitendo hivyo ni kosa la jinai.

Baadhi ya hatua zitakazochukuliwa ni wahusika kufikishwa mahakamani kwa kuwa noti na sarafu ni sehemu ya nyara za serikali. Zinapaswa kuthaminiwa.

Meneja Idara ya Uendeshaji wa BoT Tawi la Dodoma, Nalasco Maluli, alitoa angalizo hilo juzi jijini wakati akiwasilisha mada katika mafunzo ya waandishi wa habari kutoka mikoa saba ya Tanzania Bara; Iringa, Morogoro, Dodoma, Singida, Kigoma,Tabora na Njombe.

Maluli alisema fedha hizo za Tanzania ni sehemu ya tunu ya taifa, hivyo zinapaswa kuheshimiwa kama ilivyo Bendera ya Taifa na kuanzia sasa yeyote atakayebainika kufedhehesha atachukuliwa hatua za kisheria.

"Tunaomba mkaelimishe wananchi kwa kutumia vyombo vyenu kuwa fedha ya Tanzania ni tunu ya taifa, hawatakiwi kuchana wala kuharibu kwani sheria imeshapitishwa tayari, atakayebainika tunamfikisha mahakamani," alisema Maluli.

Alisema fedha hizo za Tanzania zinatengenezwa kwa gharama kubwa kwa kutumia fedha za kigeni, hivyo zinapotunzwa vizuri zitatumika kwa muda mrefu na kupunguza gharama ya kutengeneza fedha nyingine kwa kutumia fedha za kigeni.



Watuhumiwa wa kesi ya utakatishaji pesa kwa kujifanya mawakala wa Freemason wakiwa chini ya ulinzi wa askari Magereza, baada ya kufikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya kusomewa mashtaka yanayowakabili. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

## Kizimbani kwa kushawishi kujiunga Freemason

**Na Grace Gurisha**

VIJANA 12 wa wilayani Sumbawanga, mkoani Rukwa wamepandishwa kizimbani kwa mashtaka 50, likiwamo kutuma ujumbe mfupi kwenye simu za watu mbalimbali kuwashawishi wajiunge na chama cha Freemason Tanzania na kujitambulisha kuwa ni waganga wa kienyeji wanasafisha nyota.

Washtakiwa hao ni: Pius Mahali (29), dereva; Best Shinyangwe (24), dereva bodaboda; Andrea Kipeta (31), mkulima; Lusekelo Jimmy (32); Michael Donati (28); Lucas Mpanduzi (19); Steven Seleman (18); Emmanuel Kawimbe (30); Alvin Mbingi (30); Charles Selaman (20); Fabian Dismas (18) na Alex Tungombe (27), wote wakulima.

Wakili wa Serikali Eric Kamala, akisaidiana na Aaron Titus, alidai jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Romuli Mbuya wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kuwa washtakiwa wanatuhumiwa kwa mashtaka 50.

Hayo ni kuongoza genge la uhalifu, mashtaka 19 ya kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu, mashtaka 12 ya kutuma ujumbe wa simu kushawishi, mashtaka 17 ya kutumia laini zilizosajiliwa kwa majina ya watu wengine na moja la utakatishaji fedha.

Kamala alidai washtakiwa hao walitenda makosa hayo mwaka 2023 na mwaka 2024 katika maeneo yasiyofahamika ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakituma ujumbe ufupi kwenye simu za watu na kisha kujipatia fedha Sh. milioni 9.2 kutoka kwa watu mbalimbali, wakiwamo mawakala.

Alidai kuwa mahali anatuhumiwa Desemba 19, 2023 alimtumia mtu ujumbe kuwa, "Mjukuu wangu nimekusaidia sana, mpaka sasa una majumba magari ya kifahari lakini hata kuja kunishukuru hujawahi, nizirudishe mali kwenye mizimu? Basi ninakutakia utajiri mwema."

Ujumbe mwingine, mshtakiwa Shinyangwe anadaiwa kuutuma kwenda kwa Samwel Kiwembe Mei 6, 2024 kwamba, "Leo unakufa, majini yamekasirika sana."

Mshtakiwa huyo siku hiyo anadaiwa kuwa alituma ujumbe mwingine kwenye namba ya simu 0697 590... kwamba, "Binti kuna shida inakwenda kukutokea leo muda wa jioni."

Mshtakiwa watano, Kipeta anadaiwa kutuma ujumbe kwenye namba mbili tofauti akieleza kwamba, "(666) jiunge na chama huru cha Freemason Tanzania umiliki mali, pesa, majumba, mvuto, vipaji, pete bila kafara kwa kujiunga piga 0772 981316."

Kamala aliendelea kusoma ujumbe unaodaiwa kutumwa na washtakiwa, akidai mshtakiwa wa nane, Mpanduzi Machi 10, 2024 alituma ujumbe unaoeleza kuwa, "Mjukuu wa Kisile ninaona biashara ya mabasi sasa inatosha, umeshanunua mabasi mengi, sasa uje tena Sumbawanga nikupe dawa ya kusafisha nyota na ya ndagu, mimi ni babu yako wa Sumbawanga Mzee Ramadhani."

Alidai kuwa mshtakiwa Kawimbei Januari Mosi, 2024 akiwa eneo na mkoa usiofahamika ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alituma ujumbe mfupi kuwa, "Kaka ninashukuru sana kwa mtaalamu aliyeniletea kwani kwa sasa. Na ajabu leo asubuhi tumewakuta wale wezi walioiba vile vitu getini wakiwa wamevibeba vyote, sasa ninakuomba sana tena kwa ustadhi kamwambie kuwa nimpe nini kama zawadi? Pls jibu."

Baada ya washtakiwa kusomewa mashtaka hayo, hawakuruhusiwa kujibu chochote kwa sababu kesi hiyo ni ya uhujumu uchumi na pia shtaka la utakatishaji fedha halina dhamana kisheria. Mahakama ya Kisutu haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo.

Upande wa mashtaka ulidai upelelezi haujakamilika na kuomba tarehe nyingine ya kutajwa. Kesi iliahirishwa hadi Julai 27, 2024. Washtakiwa walirudishwa mahabusu.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wenye ualbino wana haki kuishi kama watu wengine

**MATUKIO** ya kutekwa kwa watu wenye ualbino yameanza kujitokeza na kuweka jamii hiyo katika hali ya wasiwasi.

Watu wenye ualbino wana haki ya kuishi kama wengine kama Katiba ya nchi inavyosema.

Hata hivyo, kumejitokeza makundi ya watu yaliyoanza kuweka maisha ya jamii hiyo kwenye wasiwasi na hata kuogopa kutembea kama binadamu wengine.

Kibaya zaidi watu hao wanawindwa hata wanapokuwa wamelala jambo linalowanyima haki ya kuishi kama binadamu wengine.

Matukio haya yanahusishwa na imani za kishirikina na baadhi ya waganga wa jadi wanatuhumiwa kuhusika katika hilo. Pia baadhi ya wafanyabiashara wanatajwa kuhusika na vitendo hivyo kwa kutaka utajiri wa haraka haraka.

Kuhusishwa kwa baadhi ya waganga wa jadi kumetokana na tabia yao ya kuwatuma wateja wao kuwawinda watu wenye ualbino kwa madai kuwa viungo vyao vikitengenezewa dawa, wafanyabiashara hao watafanikiwa kupata utajiri wa haraka haraka.

Vitendo hivi vya mauaji ya watu wenye ualbino, kukatwa viungo na kutekwa vimedaiwa vikijitokeza wakati biashara za madini zikishamiri na kila wakati inapokaribia kipindi cha uchaguzi.

Ndiyo maana kumekuwa na imani kuwa vitendo hivyo vinafanyika kwa kuamini mambo ya nguvu za giza ambazo zinawaondolea watu wasiokuwa na hatia haki ya kuishi.

Tukio la hivi karibuni la kutekwa kwa mtoto mwenye umri wa miaka miwili mwenye ualbino, limezua taharuki kubwa.

Mtoto huyo aliibiwa kijijini kwao Buamula, mkoani Kagera akiwa mikononi mwa mama yake na watu wasiojulikana na mpaka sasa haijulikani kama yuko hai au la.

Kwanini matukio kama haya yaendelee kutokea nchini kila mara, huku baadhi ya wahalifu wakikamatwa na wengine kupata adhabu kali?

Matukio haya yanasababisha watu wenye ualbino kuomba ulinzi ili wakiwa kwenye shughuli zao au wakiwa kwenye makazi yao wasiwe na wasiwasi wa kuvamiwa na kufanyiwa vitendo vibaya.

Tanzania inasifika kwa kuwa nchi yenye amani na utulivu na wananchi wake wako huru kutembea bila kuwa na wasiwasi, lakini watu wachache wenye uroho wa utajiri wanataka kuitia doa kwa vitendo vya kinyama wanavyoyowafanyia binadamu wenzao.

Pamoja na wanaharakati wanaopigania haki za binadamu kupiga kelele kuhusu matukio hayo na kutaka watu wenye ualbino wasichukuliwe kama viumbe tofauti, bado watu wenye imani potofu wanaendeleza vitendo hivyo.

Serikali kwa kushirikiana na vyama vya watu wenye ualbino vinatoa elimu ya kupambana na matukio hayo na kuna wakati hali hiyo ilitulia, lakini yameanza kujitokeza tena kutokana na baadhi ya watu kutaka utajiri wa haraka bila kufikiria uhai wa watu wengine.

Unapomuua binadamu mwenzako kwasababu ya kutaka mali, huo utajiri utakuwa na raha nao? Hivi wanaofanya vitendo hivyo wana hofu ya Mungu kweli? Watu wote wanapaswa kupaza sauti kukemea unyama huo.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kimekuwa mstari wa mbele kutetea haki za binadamu na katika tukio hili la kutekwa kwa mtoto wa miaka miwili kimetaka serikali kupitia vyombo vyake vya ulinzi, mtoto huyo apatikane.

Pia, ni muhimu kila mtu kuweka ulinzi dhidi ya mwenzake ili yanapojitokeza matukio kama hayo iwe rahisi hatua kuchukuliwa haraka.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita. 0713 578284,
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Kuiba misalaba, mashada ya maua makaburini ni laana

**KWA** miaka ya hivi karibuni kuna kukithiri kwa wizi wa mashada ya maua makaburini, na ung'oaji wa misalaba unaofanywa na baadhi ya vijana kwa lengo la kuuza vyuma chakavu.

Katika baadhi ya makaburi ambayo hayalindwi, kumekuwa na aina hiyo ya wizi hasa katika miji mikubwa kama Dar es Salaam, Arusha, lakini kwa sasa hali imeendelea kuwa mbaya, safari hii jiji la Dodoma limekumbwa na kadhia hiyo.

Katika kata ya Chang'ombe, jijini humo wamelalamika kuzuka na kukithiri kwa ung'oaji misalaba kwenye makaburi unaofanywa na baadhi ya vijana wa huko.

Wakazi hao wakasema kuwa wezi hao, wamekuwa pia wakibomoa zege na kuchukua nondo, kisha kwenda kuziuza kama chuma chakavu.

Wakasema kutokana na hali hiyo, hivi sasa baadhi ya ndugu wanaofiwa kwenye kata hiyo, wanalazimika kuweka alama za mawe kwenye makaburi ya wapendwa wao waliofariki, au misalaba ya mbao ambayo wanadai imekuwa ikiliwa na mchwa

"Inatusikitisha sana kutokana na vitendo hivyo ambavyo ni sawa na udhalilishaji wa ndugu zetu waliokufa kwa kuibiwa alama zao, ambazo ni muhimu kwa kumbukumbu kujua walikozikwa," alisema mmoja wa wakazi, Hamis Ramadhani.

Mwenyekiti wa Serikali za Mitaa Mazengo, iliyopo kata hiyo, Abdallah Mtosa, amekiri wakazi kufikisha malalamiko ofisini kwake kuomba kuwadhibiti aliowaita 'vijana'.

Akasema kuwa, watafanya kazi hiyo kwa kushirikiana na jeshi la Polisi. Akasema vijana wengi maeneo hayo wamekuwa na tabia mbaya ya kucheza kamari, kubeti, kukaa vijiweni, badala ya kutumia muda wao kufanya kazi.

Ukweli ni kwamba, tabia hii haipo Dodoma tu, kama nilivyosema imeenea maeneo mengi nchini, hasa mijini na katika makaburi ya kijamii ambayo hayalindwi.

Biashara ya chuma chakavu kwa kiasi kikubwa ndiyo imesababisha kukithiri kwa biashara hii, ambapo mbali na kung'oa misalaba, vijana ambao kwangu mimi sitakuwa na jina lingine la kuwaita zaidi ya wezi, wamekuwa pia wakirandaranda mitaani na kuimba sufuria, sahani na bakuli zilizotengenezwa kwa bati.

Pamoja na haya yote huwezi kulaumu kuwepo kwa biashara hiyo kuwa ndiyo kunasababisha hivyo.

Huwezi kukataza biashara ya visu kwa sababu eti kuna mtu amempiga mwenzake kisu, badala yake aliyefanya hivyo ndiye atabeba msalaba, kwani hakuwa na matumizi sahihi ya bidhaa hiyo.

Kwa hiyo kinachotakiwa hapa ni kudili na wezi hao, na si kupiga marufuku biashara ya chuma chakavu.

Nasema hivi kwa sababu baadhi ya watu wataona kama ni hivyo basi biashara hiyo ipigwe marufuku, la hasha. Cha kufanya ni Jeshi la Polisi, Polisi Jamii na Wananchi wote kwa ujumla wote nchi nzima wawe macho na wahalifu hawa.

Kinachosikitisha ni kwamba baada ya vijana wanaofanya uhalifu huo wanafahamika ni wa hapo hapo mitaani, lakini hawakamatwi si kama hawajulikani, lakini damu nzito kuliko maji, ni vijana wetu, na wengine wanaogopa lawama kwa majirani zao wakiwataja au kuwakamata.

Na si misalaba tu, imefika wakati wanasubiri watu waondoke makaburini, wanakwenda kuzoa mashada ya maua ambayo yamewekwa na kwenda kuyauza.

Nimezunguka kote, lakini narejea kuwakanya, kuwaambia na kuwatahadharisha vijana wenye tabia hiyo, kuwa pamoja na kwamba ni uhalifu kama mwingine wowote, hivyo ni kosa la jinai, lakini kwa utamaduni wa Kiafrika na dini zote, kuiba kitu cha mtu aliyefariki, au kuiba kitu chochote makaburini ni dhambi kubwa isiyosameheka mbele za Mungu na ni laana.

Inawezekana hata huko mbele ya safari kwenye maisha kijana akaacha mambo hayo, akawa na familia, lakini asiwe na bahati yoyote, bali ni mikosi kila kukicha, kumbe inatokana na laana ya miaka mingi iliyopita ya kuiba makaburini.

# Vyuo 40 Tanzania kushirikiana na vya China

**Na Joseph Mwendapole**

VYUO 40 vya elimu ya ufundi stadi vya Tanzania na vyuo vinane kutoka China vimesaini makubaliano ya ushirikiano wa kuendeleza ujuzi na vyuo vya ufundi stadi vya Tanzania.

Makubaliano hayo yalisainiwa jana na wawakilishi wa vyuo hivyo mbele ya Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Profesa James Mdoe.

Walisaini makubaliano hayo kwenye kongamano lililoandaliwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET).

Akizungumza baada ya kusaini makubaliano hayo, Profesa Mdoe alisema kongalamo hilo ni mwendelezo wa ushirikiano katika elimu ya fundi.

Alisema kupitia ushirikiano huo hufanya makongamano mbalimbali yanayovikutanisha vyuo vya ufundi China na Tanzania na hilo ni kongamano la nne.

"Lengo kubwa ni kuendeleza eneo la ufundi stadi kwani wenzetu China wako mbali sana kwenye eneo la ufundi stadi na ndiyo sababu tunapata bidhaa nyingi sana kutoka China na bidhaa zingine zinatengenezwa kwenye viwanda vidogo vidogo sana," alisema Profesa Mdoe.

Alisema serikali ilitafuta ushirikiano huo ili ione namna ya kupata uzoefu kutoka China wa kuendeleza ufundi stadi ili uzoefu huo utumike kwenye uzalishaji wa bidhaa mbalimbali kwa vijana.

Alisema ushirikiano huo umeshaonyesha matunda mengi wapo wafanyakazi wa NACTVET ambao wameshakwenda China kujifunza ufundi stadi na wakati mwingine China inaleta wataalamu wake hapa nchini.

"Katika ushirikiano huu kuna makubaliano baina ya vyuo na vyuo leo tumeshuhudia makubaliano ambayo watabadilishana walimu, wanafunzi kwenda kule kujifunza kwa muda mfupi na hata kubadilishana teknolojia na utafiti mbalimbali kwa hiyo ni ushirikiano wenye manufaa makubwa," alisema.

Alisema kwenye ushirikiano huo Tanzania ndiyo imekuwa mnufaika mkubwa kutokana na teknolojia yake kuwa iko chini kulinganisha na China ambayo imepiga hatua kubwa. Alisema Tanzania inarasilimali nyingi ambazo bado hazijafanyiwa kazi hivyo wanapokuja wataalamu wa elimu ya ufundi kutoka China wanawafundisha wenzao wa Tanzania namna ya kuzitumia kupata bidhaa.

Alisema Tanzania imekuwa ikitumia fursa ya ushirikiano huo kuwapa mafunzo wakufunzi wa vyuo vya ufundi ili wapate teknolojia ya juu ya kuendeleza vyuo vyake hapa nchini.



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. James Mdoe (wa tatu kushoto), akizindua ushirikiano wa vyuo 40 vya Tanzania na vyuo nane vya China wakati wa kutiliana saini mkataba wa ushirikiano, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Dk. Nchimbi ampa kibarua Makonda kero za wananchi

**Na Romana Mallya,** ARUSHA

WANANCHI 350 jijini Arusha wamewasilisha kero mbalimbali mbele ya Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, ambaye amemwagiza Mkuu wa mkoa huo, Paul Makonda, kwenda kuzitatua kwa kupita kata kwa kata.

Alitoa maelekezo hayo juzi jijini hapa wakati wa mkutano wa hadhara ikiwa ni mwendelezo wa ziara yake ya kuzungukia mikoa mitano kutatua kero za wananchi na kuangalia utelezaji wa ilani.

Balozi Nchimbi alimwagiza Makonda apite kata kwa kata kuzitatua kero za wananchi mkoani humo.

"Tumekubaliana na Mkuu wa mkoa afanye ziara kata kwa kata kwa ajenda ya kero tu. Bahati nzuri tunamwamini Mkuu wa mkoa," alisema.

Naye, Makonda aliahidi kutekeleza agizo hilo ili wananchi waendelee kuwa na furaha ya Chama cha Mapinduzi.

"Tumepokea na tutatekeleza kwa ubunifu mkubwa," alisema Makonda.

Katika hatua nyingine, Makonda aliomba kupewa miezi sita ya kusafisha mkoa huo kisha ahamishwe kwingine.



Alisema ifikapo Januari mosi, 2025, Arusha itakuwa namba moja kwa kila kitu kwa kuwa wana kila sababu ya kufanikiwa.

"Nakupa tu mfano mdogo Halmashauri ya Jiji la Arusha mwaka 2023/24, walimwomba Rais Samia Suluhu Hassan, zaidi ya Shilingi bilioni saba na amewaletea asilimia 98, cha kusikitisha fedha waliyotumia ni Sh. milioni 500 tu, wana takribani Shilingi bilioni saba hawajatumia," alisema.

Alisema ni fedha ambazo Rais aliwapa ili wananchi wa Arusha wapate maendeleo, ambapo mapato ya ndani waliyokusanya ni takriban Sh. bilioni 30 na fedha waliyotumia haizidi Shilingi bilioni nne.

"Jumla ya Sh. bilioni 20 huenda zikarudi mpaka mwaka mwingine wa fedha wakati wananchi wanalia hawana maji, kuna watoto wanakaa chini hawana madarasa, kuna maeneo barabara hazipitiki.

"Hili suala si la Rais Samia au CCM niachieni kwenye huu mkoa niwanyooshe mpaka waseme kazi waliyotakiwa kufanya. Takwimu hizi si zangu nimezipata kwa Mkuu wa wilaya, alisema Makonda.

"Nakuhakikishia hakutakuwa na jiwe litakalosalia juu ya jiwe lazima maendeleo yaliyopangwa na ilani ya CCM yafike kwa kila mwananchi Arusha.

## KABWELA

**Na Fadhil Mohammed**



# Wafanyabiashara walalamika makali gharama usafirishaji

**Na Jenifer Gilla**

WAFANYABIASHARA wanaoagiza mizigo kutoka China wamelalamikia kupanda kwa gharama za ushuru wa kusafirishia mizigo hapa nchini kutoka kwa kampuni za usafirishaji.

Wakizungumza na mwandishi wa gazeti hili jana waliomba serikali kushughulikia tatizo linalochochea kupanda kwa gharama hizo kwa kuwa hali ikiendelea hivyo watalazimika kupandisha bei ya bidhaa ili kufidia.

Mfanyabiashara wa nguo za kike, Beatha James, alisema kuwa wiki iliopita alikwenda kuchukua mzigo wake kwa wakala wa usafirishaji na kutozwa Sh. 2700 kwa gauni moja kutoka Sh. 1700 gharama za awali.

Alisema ongezeko hilo linaathiri mapato katika biashara yake kwa kuwa analazimika kuza bei iliyozoeleka kwa wateja kwa ajili ya kulinda soko lake.

"Kwa sasa hivi ukisema upandishe bei utapoteza wateja kwa sababu kuna wenzako wengi hawajapandisha bei, kwa hiyo inabidi nikubali kuathiri kipato changu kwa sasa wakati nasubiria serikali inatafanya nini," alisema.

Mfanyabiashara wa viatu, Deo Shayo, alisema ametozwa Sh. 2800 kwa kila kiatu kutoka Sh. 2000 jambo litanaloathiri biashara yake kwa kuwa ni vigumu kupandisha bei peke yake kwa sasa.

Aliiomba serikali kukaa pamoja na wasafirishaji ili kuona namna gani wanaweza kupunguza gharama hizo zisiendelee kuwaumiza kwa kuwa hali ikiendelea hivyo watalazimika kupandisha bei.

Mfanyabiashara wa pochi na viatu, Hapiness Shirima alisema amelazimika kutouza mzigo wake wa pochi alioupokea wiki mbili zilizopita akisubiria kama wenzake watapandisha bei auze pamoja nao kufidia gharama za usafiri zilizoongezeka.

Akizungumza katika kituo cha habari Mei 21, mwaka huu, Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchukuzi, Prof. Godius Kahyarara, alikiri kuongezeka kwa gharama hizo na kuahidi kuwa serikali inafanya jitihada kukabiliana na changamoto hiyo.

Alisema wanafanya mikakati mbalimbali ili kukabiliana na changamoto hiyo ikiwamo kuongeza kasi ya kuondoa mizigo bandarini ili kupunguza gharama za uendeshaji na kuongeza miundombinu ya kusafirisha mizigo toka bandarini.

Alisema kwa kushirikiana wa wadau wa usafirishaji wamekubaliana kutafuta kampuni zitakazoweza kusaidia meli zinazounganisha mizigo inayokuja Tanzania.

Mkurugenzi wa Jumuia ya wafanyabiashara wa Kariakoo (JWK), Martin Mbwana, alisema dalili njema zimeanza kuonekana baada ya kampuni za usafirishaji kuanza kushusha gharama.

Alitoa mfano tangu wiki iliyopita gharama za kusafirisha kontena la futi 40 zilishuka kufikia Dola za Kimarekani 7000 (Sh. milioni 18) toka Dola 9000 (Sh. milioni 20.3).

Alisema baada ya gharama hizo kupanda waliiomba serikali ipunguze gharama ya bima na usafirishaji ili ushuru usiwe mkubwa na kumuumiza mtumiaji wa mwisho.

"Tukaomba angalau bei ya usafirishaji ibaki palepale angalu dola 2500 hado 3000 ambayo tumeizoea ili isiwe kubwa sana tushindwa kukidhi mahitaji ya soko na mlaji wa mwisho akapandishiwa bei," alisema Mbwana.

Kuongezeka kwa gharama za usafirishaji kunaelezwa kusababishwa na meli kutoka bara la Asia kupita njia ndefu ya Afrika Kusini wakikwepa njia fupi ya Suez Canal ambako kunaelezwa kuwa na uharamia.

Sababu nyingine inaelezwa kuwa ni uhaba wa meli ambazo nyingi zinaelekea bara la Ulaya pamoja na uhaba wa kontena za kubeba mizigo.




Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), Dk. Erasmus Kipesha akitoa maelezo kuhusu majukumu ya TEA kwa Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Balozi Dk. Batilda Burian alipotembelea maadhimisho ya Wiki ya Elimu, Ujuzi na Ubunifu yanayofanyika kwenye viwanja vya Shule ya Sekondari Popatlal, jijini Tanga mapema wiki hii. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

## Miaka 20 jela kukutwa na nyama ya swala

**Na Judith Julius,** NGARA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Wilaya ya Ngara Mkoa wa Kagera, imewahukumu watu wawili kifungo cha miaka 20 jela kila mmoja kwa kosa la uhujumu uchumi.

Washtakiwa hao ni Gabagambe Itwaza (48) na Ijenela Emmanuel (23), wakazi wa kijiji cha Kamli kilichopo wilayani Ngara.

Hakimu Emmanuela Kavalo wa mahakama hiyo akitoa hukumu hiyo, alisema mahakama imeridhishwa na ushahidi uliotolewa na upande wa Jamhuri na kubainisha kuwa kila mmoja atatumikia kifungo cha miaka 20.

Awali, Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Lawrence Liwanda, alidai washtakiwa hao walikamatwa Mei 22, 2023 ndani ya Hifadhi ya Buligi, Chato iliyopo kwenye eneo la kijiji cha Kamli. Washtakiwa hao walikamatwa wakiwa na nyama pori ya swala yenye thamani ya Sh. 1,070,700.

Liwanda alibainisha kuwa walikamatwa kwa kosa la kuingia ndani ya hifadhi bila kibali na kumdhulumu swala uhai wake.

Katika utetezi wao, washtakiwa hao waliomba kusamehewa kwa maelezo kuwa wanategemewa na familia zao.

Mwendesha mashtaka, Liwanda, aliiomba mahakama itoe adhabu kali kwa mujibu wa sheria ili iwe fundisho kwao na kwa wengine ambao wanajihusisha na vitendo hivyo.

# Ubelgiji yajivunia ushirikiano miaka 40 na Tanzania

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

BALOZI wa Ubelgiji nchini Tanzania, Peter Van Acker amesema nchi yake inajivunia kuwa na ushirikiano mzuri na Serikali ya Tanzania kwa miaka 40 katika nyanja ya uchumi, afya, maji na elimu na itaendelea kudumisha diplomasia pamoja na kuunga mkono jitihada za serikali kusimamia uwiano wa jinsia na demokrasia na utawala bora.

Balozi Van Acker amesema mafanikio hayo yanatokana na Umoja wa Vyuo vikuu vya nchini Ubelgiji na Chuo Kikuu Mzumbe(MU), wilayani Mvomero, Mkoa wa Morogoro kuwa na ushirikiano kwa kipindi cha miaka 10 katika utekelezaji wa programu za kitaaluma kwa kufanya utafiti na kuzitatufitia ufumbuzi changamoto zilizopo kwenye jamii, elimu ya ujasiriamali na upatikanaji wa huduma ya majisafi.

Alisema hayo kwenye hafla ya kufunga programu hiyo ya miaka 10 iliyofanyika katika Chuo Kikuu cha Mzumbe iliyowashirikisha viongozi mbalimbali wa serikali na uongozi wa Chuo Kikuu cha Mzumbe.

Alisema kuwa nchi yake kupitia ushirikiano wa utafiti mbalimbali imesaidia Serikali ya Tanzania katika mipango yake ya kusaidia kwenye nyanja za kiuchumi, afya, maji na elimu kupitia miradi mbalimbali waliofadhili.

"Kukamilika kwa pragramu hii sio mwisho bali ushirikiano kati ya Chuo Kikuu cha Mzumbe na Ubelgiji katika masuala ya kitaaluma utaendelea kwa kutoa ufadhili katika kufanya utafiti mbalimbali utakaosaidia jamii kwenye maendeleo yao," alisema.

Akifunga programu hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Mvomero, Judith Nguli, kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Morogoro Adam Malima, alipongeza jitihada zinazofanywa na Ubelgiji katika kusaidia programu hiyo ya kufanya utafiti wa masuala ya kitaaluma na kijamii na kutaka uendelee katika wilaya nyingine za Mkoa wa Morogoro.

Aliutaka uongozi wa Mzumbe kutoa elimu kwa wananchi kuhusu masuala ya demokrasia na utawala bora kwa viongozi wa serikali za mitaa waliopo madarakani na ambao watakachaguliwa katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika mwaka huu.

Alisema kuwa kazi inayofanywa na Chuo Kikuu cha Mzumbe ni kubwa na serikali ina matumaini makubwa na chuo hicho katika kusaidia kutoa maarifa na ujuzi katika masuala ya uongozi kwa watu.

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Mzumbe, Profesa William Mwegoha, alisema mradi huo unaotekelezwa na umoja wa vyuo vilivyopo Ubelgiji, umekuwa na manufaa makubwa kwa Chuo cha Mzumbe na serikali kwa ujumla.

Alisema moja ya mafanikio hayo ni pamoja na kupanuka kitaaluma kwa wanataaluma 12 kuhitimu shahada za Uzamivu kwa kufanikisha malengo ya kimkakati ya chuo katika masuala ya Tehama kutengeneza mitaala na kuboresha njia ya ufundishaji.

Alitaja maeneo mengine yaliyoleta tija kupitia mradi huo ni kuwa na wataalamu wenye ubobezi kwenye ubunifu katika ufundishaji na tija kwa chuo na jamii kwa ujumla.



## Neema wanyamapori yavishukia vijiji

**Na Godfrey Mushi,** LONGIDO

VIJIJI vya Irkaswa, Kitendeni, Lerang'wa na Kamwanga wilayani hapa Mkoa wa Arusha vimeanza kuonja matunda ya kiuchumi yanayotokana na ulinzi wa ushoroba wa Kitendeni wa mapito ya wanyamapori wanaohama kati ya Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro na Amboseli ya nchini Kenya.

Jana, Msimamizi wa Mradi wa SOKNOT (Southern Kenya, Northern Tanzania) ulioko chini ya Shirika la World Wildlife Fund (WWF), Profesa Noah Sitati alieleza Nipashe kuwa vijiji hivyo ambavyo ni wanachama Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori ya Enduimet (EWMA), vimeanza kunufaika kwa kupata motisha ya utunzaji na ulinzi wa ushoroba huo.

" Julai mwaka 2023, WWF iliutambulisha mradi wake mpya wa majaribio wa miezi 18 wa Wildlife Credit, maarufu kama tuzo, unaolenga zaidi kutoa motisha ya utunzaji na ulinzi wa Ushoroba wa Kitendeni.

Hii ni kwa sababu, Ushoroba wa Kitendeni ni muhimu kwa kuwa tembo wanatumia na wanyama wengine kutoka kule Amboseli, Kenya mpaka Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro.

"Mnajua ushoroba wa Kitendeni ni muhimu kwa kuwa tembo wanatumia na wanyama wengine kutoka kule Amboseli, Kenya mpaka Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro. Tunataka mradi huu utoe picha na matokeo halisi kabla ya kutekelezwa katika jumuiya nyingine zote za uhifadhi nchini Tanzania.

...Ni kama tuzo fulani ya kusema hongereni kwa kutunza hii corridor (shoroba) isikae wazi; kwa vile hakuna maendeleo kule ndani. Tunatafuta namna ambayo jamii, inaweza kufaidi na ndio maana tukatengeneza huu mradi mdogo wa majaribio, ambao unakuja kusaidia jamii iliyojikita kuilinda corridor ya Kitendeni."

Kwa mujibu wa Prof. Sitati, moja ya vigezo vilivyotumika kuonyesha kijiji kimefanikiwa kutunza na kulinda ushoroba huo ni kuzuia ujenzi wa makazi, shughuli za kilimo, ujangili au uwindaji haramu wa wanyamapori.

"Kuna mambo mengi ambayo yanaweza kuharibu corridor, kwa mfano kuna majangili wanaweza kuingia na kuua wanyama wakipita, lakini nyie wenyewe ndio macho kwa vile mnajua hiyo ni sehemu yenu.

"Kuna wale watu wanachoma mkaa, ama wanakata miti kama mbao. Wanachukua mali yenu wanapeleka kwingineko. Nasikia upande wa Kenya, majangili wanaua wanyama, na hao wanyama ndio wanaoleta utalii katika sehemu yetu ya Enduimet WMA. Tunaita photographic tourism."

Mkazi wa Kijiji cha Irkaswa, Sinyoki Melita, alieleza furaha yake namna mradi huo unavyokwenda kuchochea na kuinua maisha yao kiuchumi kutokana na kuwapo kwa ushoroba huo.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Kamwanga, Juma Mohamed, amewaonya wakazi wa kijiji hicho kuacha tabia ya kuua na kula wanyamapori kuanzia sasa kwa kuwa kigezo hicho kitawanyima fursa ya kunufaika na fedha zinazotolewa kutokana na mradi wa Wildlife Credit.

# Watupa nyenzo, waacha ungariba

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

WANAWAKE mashuhuri 80 wa jamii ya kifugaji ya Kimasai wilayani hapa Mkoa wa Kilimanjaro wametangaza kuachana na mila potofu ya kukeketa watoto wachanga na wasichana katika familia zao ili kuheshimu haki za msingi za binadamu.

Uamuzi huo unatokana na kufikiwa watu 3,503 na kampeni ya kupambana na ukeketaji katika koo za jamii hiyo inayoendeshwa na Taasisi ya Kimataifa ya Friedrich Naumann Foundation for Freedom (FNF).

Ngariba mstaafu, Kinini Lukumay, ambaye ametangaza kuachana na kazi hiyo na kuwa kinara wa vita dhidi ya ukeketaji, alisema katika Kata ya Donyomurwa, vijiji vya Embukoi, Donyomoruwa, Munge na Loiwang,

vimeachana na mila hiyo baada ya kupata elimu ya madhara ya ukeketaji.

Vijiji hivyo pia vimetunga na kupitisha sheria ndogo inayong'ata zaidi familia za kifugaji zinazopokea 'sukari' kwa ajili ya kuozesha watoto wenye umri mdogo, kupinga ukeketaji na ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto.

Ukeketaji ni uondoaji wa sehemu za siri za mwanamke, na ni kitendo chochote kinachoharibu maumbile kutokana na sababu ambazo sio za kimatibabu.

Ofisa Mradi wa Haki za Binadamu Pamoja na Jinsia wa Shirika lisilo la Kiserikali la KWIECO, Elizabeth Mushi, alisema wanafanyakazi ya kuzijengea uwezo jamii za kifugaji wilayani hapa kupinga vitendo hivyo kupitia mradi wa jamii salama.

Alisema hadi sasa, wananchi wa jamii ya kifugaji ya Kimasai 3,503, kati yao wanaume 1,301 na wanawake 2,202, wamefikiwa na kampeni hiyo ya kupinga ukeketaji na mimba za utotoni.

"Kwa mujibu wa viongozi wa mila wa jamii ya Kimasai, kupata elimu kwa jamii hiyo katika Wilaya ya Siha kumesaidia kuwanusuru watoto wa kike 718 waliokuwa kwenye hatari ya kukeketwa wakati sherehe za kimila," alisema.

Mkuu wa Divisheni ya Maendeleo ya Jamii ya Wilaya hiyo, Marko Masue, alisema: "Kama serikali tumeamua kukemea, kupinga ukeketaji, ndoa za utotoni, kuozesha watoto na vitendo vyovyote vya ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto.

"Kimsingi, ukeketaji unaumiza wanawake na wasichana kimaungo na kiakili, na hakuna faida yoyote ya kitabibu wakati wa kitendo hicho.

...Zaidi ya kuchangia huzuni, na kuharibu uhusiano wa wanawake na vile wanavyojihisi."

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, amewahi kunukuliwa akisisitiza kwa kuwa baadhi ya mangariba wanatishiwa, na hata kutengwa na jamii zao baada ya kuacha vitendo hivyo vya kikatili, serikali itawalinda na kuwatetea kwa nguvu zote bila kuchoka.



Mwenyekiti wa Umoja wa Wazazi wa CCM Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Hatibu Bakari (kulia), akijadiliana jambo na wajumbe, walipotembelea kukagua Shule ya Sekondari ya Wazazi iliyopo Mbaramo, wilayani humo juzi, iliyosimama kutoa huduma kwa muda mrefu pamoja na kukagua ujenzi wa nyumba mpya ya Katibu wa Wazazi wilaya hiyo. Wa pili kulia ni Katibu wa Wazazi wa Wilaya ya Muheza, Nachia Juma Ali. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Kimbunga kusomba vijana walevi, wauza gongo

**Na Mary Mosha,** MOSHI

SERIKALI wilayani hapa Mkoa wa Kilimanjaro imeanzisha operesheni ya kupambana na ulevi wa kupindukia dhidi ya vijana ili kulinda nguvu kazi ya taifa.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Wilaya hiyo, Zephania Sumaye, operesheni hiyo ya siku 21, imebatizwa jina la 'Rudisha Moshi katika hali yake, tokomeza ulevi uliopitiliza.'

Kwa mujibu wa Sumaye, operesheni hiyo, pamoja na mambo mengine, mbwa wenye mafunzo maalumu watatumika kunusa na kutafuta watengenezaji wa pombe haramu aina ya gongo na wauzaji mitaani.

Akizungumza na madiwani na watendaji katika kikao cha kawaida cha Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Moshi alisema kuwa: "Tunafanya hivi kwa sababu, tumebaini vijana wengi wanashindwa kufanya shughuli za maendeleo katika jamii. Siku ya kwanza katika eneo la Uru Shimbwe (Kibosho), zilimwagwa pipa tisa za molalesi zilizokuwa zimeandaliwa kwa ajili ya kutengeneza gongo.

"Viko viwanda vinne, ila wamiliki wawili bado hawajakamatwa. Vijana wangu wapo timamu tunatumia hadi teknolojia ya mbwa katika kunusa na kutafuta, siku 21 hizi zitakuwa za giza na nyeusi, madiwani naomba mniunge mkono kwa kutupa taarifa sahihi.

Sumaye, alisema operesheni hiyo siyo kwa waandaaji na wauzaji wa pombe haramu pekee, bali na hata kwa wale wauzaji wa maduka ya mangi ya vileo tishio kwa afya.

"Nimetoa maelekezo, vilabu vyote vya pombe vitafunguliwa kuanzia saa 9:30 mchana hadi saa 10:00 jioni, lakini kwa siku za kazi na wikiendi (mwisho wa juma) vitafungwa saa 6:00 usiku.

...Nendeni mkawaambie kuna kimbunga kinakuja kisiwakute. Hatutalala mpaka tuokoe kizazi cha vijana wa Moshi. Nina fahamu na ninajua watawafuata wakitishia kuwanyima kura, ila kwa hili naomba wasikilizeni ila niacheni nifanye kazi," alisisitiza Mkuu wa Wilaya.

Alisema Moshi ina misingi imara iliyowekwa na watangulizi wake, hasa kwenye sekta ya elimu, kukuza uchumi na uwajibikaji kwa maisha binafsi kwa kuwa vijana wake wamesambaa Tanzania nzima kwa asilimia 70 na wana uchumi imara. Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Moris Makoi, alitoa rai kwa madiwani, watendaji wa kata na vijiji kulichukulia jambo hilo kwa mapana, kutoa ushirikiano na kuwaelimisha wafanyabiashara kutokomeza ulevi.

"Ikiwa jambo hili litatekelezeka kwa vitendo, linaweza kuleta matokeo chanya na kubadilisha kizazi cha jamii ya Moshi," alisema Diwani wa Mwika Kaskazini, Samweli Shayo.





# Fisi watishia maisha 'wahemea' maji mtoni

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKAZI wa Kata ya Uyogo Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga wanaoishi jirani na Hifadhi ya Moyowosi Kigosi wako hatarini kushambuliwa na fisi wanapokwenda mtoni kuteka maji.

Hayo yalisemwa na Diwani wa Viti Maalumu Kata ya Uyogo, Asha Michael wakati akizungumza kero ya ukosefu wa maji inayowakabili wakazi hao na wengine wa halmashauri hiyo.

Asha, alisema wakazi hao wanalazimika kuamka alfajiri kwenda mtoni kuwahi maji yasichafuliwe na wanyama hao wakiwamo fisi.

Alisema wakazi hao wanalazimika kwenda kwa makundi katika mto huo kwenda kuteka maji ili kunusuru maisha yao.

Alisema wakati wa kiangazi visima na mabwawa walivyochimba kando ya makazi yao vinakauka, hivyo kulazimika kutembea umbali mrefu kwenda kata za jirani zenye maji ya uhakika.

Jiografia ya Ushetu ina maeneo ya miamba, hakuna maji licha ya Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA) kufanya juhudi za kutafuta maji kwa lengo la kuwaondolea wakazi hao adha hiyo.

Mkurugezi Mkuu wa RUWASA, Clement Kivegalo, alisema wakazi hao na wengine wa Ushetu wataondokana na adha hiyo baada ya Serikali kutoa Sh. bilioni 44.2 kwa ajili ya kusambaza maji katika maeneo yao ya Ziwa Victoria, kutoka Manispaa ya Kahama hadi Ushetu.

Kwa mujibu wa Kivegalo, mradi huo unatajiwa kukamilika ndani ya miezi 22 baada ya mkataba wake kusainiwa siku chache zilizopita katika Kata ya Ulowa.

Hafla ya kusaini mkataba huo, ilihudhuliwa na Waziri wa Maji Juma Aweso na Waziri wa Fedha, Dk. Mwiguli Nchemba.

Mradi huo utakuwa na matangi matatu yenye ujazo wa lita 500,000, jingine 300,000 na 100,000 katika maeneo tofauti.

Mradi huo ambao utahudumia zaidi ya wakazi 189, 836, utasimamiwa na RUWASA.

Awali Mbunge wa Ushetu, Emmanuel Charahani, alijivunia ujengaji hoja bungeni kuwa umesababisha kupata mradi mkubwa wa maji hayo ya Ziwa Victoria.

Charahani, aliwataka wakazi hao kuwa walinzi wa vifaa kazi vitakavyoletwa na makandarasi katika utekelezaji wa mradi huo.

## W'biashara walilia uzio mnadani

**Na Elizabeth Seleman,** SENGEREMA

WAFANYABIASHARA wa mifugo katika mnada wa ng'ombe uliopo Kata ya Sima wilayani hapa Mkoa wa Mwanza wameiomba serikali kujenga uzio kwa ajili ya kuwadhibiti wanaokwepa kulipa kodi.


Wakizungumza kwa nyakati tofauti, wafanyabiashara hao walidai kuwa baadhi yao wamekuwa hawapiti kwenye mlango wa kuingia mnadani kwa kisingizio kuwa wana ng'ombe mmoja au wawili, hivyo kukwepa kulipa kodi.

"Uzio uliopo ni waya na umeisha chakaa, unajikunja na kukatika unapoguswa na pembe za ng'ombe, wafanyabiashara wenzetu wasio waaminifu wanatumia mwanya huo kutorosha mifugo na kukwepa kulipa kodi," alisema Sospeter Ndaki kwa niaba ya wenzake.

Ndaki, alisema wakati wa kipindi cha masika, ng'ombe wanavamia mazao na kusababisha kutozwa kiwango kikubwa cha faini kulipa fidia ya uharibifu wa kwa wakulima kutokana na kukosekana kwa uzio.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema, Yanga Makanga, alisema wameanza ujenzi wa msingi uzio huo na kuwataka wafanyabiashara hao wawe watulivu.

Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi, Photunatus Nzwangi, alisema bajeti iliyotengwa kwa ajili ya ujenzi wa uzio huo ni Sh. milioni 70 na kwamba wanasubiri ipitishwe.




Waziri wa Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa (katikati), akipokea hati ya shukrani kwa niaba ya nchi kutoka kwa Rais wa Kamisheni ya Usafiri wa Anga Afrika (AFCAC), Silas Udahemuka, ikiwa ni ishara ya kuipongeza na kuishukuru Tanzania kwa kuwa mwenyeji wa Mkutano wa pili wa Kamisheni hiyo unaowakutanisha wakurugenzi wakuu wa Taasisi za Usafiri wa Anga Afrika jijini Arusha jana. Kulia ni Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), Hamza Johari. **PICHA: DICKSON MULASHANI**

# 'Maabara kupunguza maambukizi Ukimwi'

**Na Rose Jacob,** MWANZA

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, Said Mtanda ameonyesha matumaini yake ya kuwapo kwa maabara ya uchunguzi na kupima usugu wa dawa za kufubaza Virusi Vya Ukimwi (VVU) katika Hospitali ya Rufani ya Bugando mkoani hapa kuwa kutasaidia kupunguza maambukizi ya virusi hivyo.

Akizungumza jijini hapa wakati wa makabidhiano ya maabara hiyo, Mtanda, aliwashukuru wahisani kwa kusaidia juhudi za kupunguza maambukizi hayo kwa vifaa na rasilimali watu.

" Maabara hii, itasaidia kupima vimelea na maambukizi, kutoa dira kwa afua za kuzuia maambukizi ya UKIMWI na mikoa ya Kanda ya Ziwa wamepata sehemu mahususi kwa tiba na uchunguzi, wananchi wasibweteke na kushindwa kujilinda, kujikinga na maambukizi mapya, hususani vijana kuanzia miaka 14 hadi umri wa wazee, ndiyo wanaokumbwa na tatizo hili," alisema.

Kwa mujibu wa mkuu huyo wa mkoa, misaada mbalimbali imesaidia juhudi za serikali za kupunguza maambukizi ya Ukimwi nchini.

Mkurugenzi wa Bugando, Dk. Fabian Masaga, aliwashukuru wahisani kwa kuwaboreshea maabara ya kisasa, rasilimali watu na kusaidia kupunguza matumizi ya nishati ya umeme na maji.

"Bugando ina maono ya kukomesha magonjwa ya kuambukizwa, msaada wa maabara hii utasaidia juhudi hizo za kuboresha miundombinu, wamewajengea uwezo watumishi wa maabara, ninaimani wana Mwanza na wananchi wa Kanda ya Ziwa watapata huduma bora," alisema Dk. Masaga.

**Mkurugenzi wa ICAP nchini, Haruka Maruyama, aliushukuru uongozi wa mkoa na Bugando kwa kukubali uwepo wa miundombinu hiyo muhimu kwa ajili ya kupima magonjwa kwa Watanzania kwani itasaidia kuboresha huduma hizo kwenye ukanda wa ziwa.**

Mganga Mkuu wa Mkoa huo, Thomas Rutachunzibwa, alibainisha furaha ya sekta ya afya kwa kushirikiana na wahisani hao kwenye utaalamu na miundombinu ya kufubaza virusi hivyo.

Mkurugenzi wa ICAP nchini, Haruka Maruyama, aliushukuru uongozi wa mkoa na Bugando kwa kukubali uwepo wa miundombinu hiyo muhimu kwa ajili ya kupima magonjwa kwa Watanzania kwani itasaidia kuboresha huduma hizo kwenye ukanda wa ziwa.


Akimwakilisha Balozi wa Marekani Tanzania, Mtendaji wa CDC nchini, Dk. Mahesh Swaminathan, alisema wanayo furaha kuwepo kwa miaka 15 na kusaidia takribani Sh. bilioni 4 kutekeleza mradi huo.

ama
ALHAMISI JUNI 6, 2024
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

**Waziri Ummy aingia vitani binti apige hatua kuiona hedhi salama**



**NEMC, wadau Dar walalamika wako njia panda zama kutenganisha taka**

Ukurasa 13

# Rais anavyopambana safari kufikia nishati safi kwa Watanzania 80%

## •Majaliwa, Biteko wafunguka uchochoro wanakopitia...

**Na Mwandishi Wetu**

SASA vita ilivyo kitaifa ni kuondoka kwenye matumizi ya nishati isiyo bora nchini.

Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, ametaja kuwapo zaidi ya Waafrika milioni 900 wanaotumia nishati isiyo safi kupikia, hata inachangia kuharibika mazingira, kupotea baioanuai na athari za kiafya.

Hapo anaorodhesha maeneo makuu matatu ya nishati safi, akianza na vijijini kwenye uwezo mdogo kutokana na gharama kubwa na upatikanaji wa shida.

Vilevile akataja duniani kwa jumla, hapajapewa kipaumbele suala hilo, kukiwapo ufadhili mdogo na watu kutokujua fursa za kiuchumi kwenye nishati safi, ambayo sasa inarejesha nyuma harakati hizo; huku kukiwapo ushirikiano mdogo katika ukuzaji nishati safi.

Rais Dk. Samia anasisitiza Tanzania inadhamiria kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Nishati Safi ya Kupikia uliozinduliwa hivi karibuni, kuwafikia asilimia 80 ya wananchi wanaotumia nishati hiyo ifikapo mwaka 2034.

Kwa Bara la Afrika, malengo ni kuhakikisha Afrika inapata uelewa na inakuwa jambo lao kimataifa, kutekeleza azma hiyo.

Pia, kuna suala la kuandaa sera madhumuni inayotekelezeka kwa ajili ya nishati safi kupikia na kuharakisha ushirikiano wa wadau, ikikadiriwa hitaji la Dola za Marekani bilioni 4 (Sh. Trilioni 10.584) kila mwaka, kufanikisha upatikanaji wa nishati safi hiyo kwa Waafrika wote, ifikapo mwaka 2030.



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akipanda mti wa kulinda mazingira. **PICHA: MTANDAO.**

Nchini, Rais ameziagiza wizara, taasisi, mamlaka, wadau na sekta binafsi, kuzingatia matumizi ya nishati safi ya kupikia, ili kulinda mazingira na athari za nishati isiyo safi.

Ilikuwa agizo lake Rais, tarehe 8, mwezi huu, akiwa Dar es Salaam, wakati akizindua mkakati wa Nishati Safi ya Kupikia 2024 - 2034.

Akaagiza: "Wizara ya Nishati ihakikishe inafikisha mkakati huu kwa wadau wote muhimu kwa kutumia njia rasmi. Mkakati uwe kwa lugha zote za Kingereza na Kiswahili na uwekwe katika mitandao, ili kusaidia wananchi waweze kuipata kwa urahisi.

"Mkutane na sekta zingine na kubaini maeneo ya kufanyia kazi ili kuweka bei himilivu kwa wananchi ili waweze kutumia Nishati Safi ya Kupikia."

Maelekezo mengine Dk. Samia ni kwamba: "Mkakati uonekane kwenye Dira ya Taifa ya mwaka 2050, TAMISEMI iboreshe mikataba kati yake na wakuu wa mikoa, wafanye hivyo kwa wakuu wa wilaya, ili kuhimiza matumizi ya nishati safi ya kupikia."

**MAELEKEZO KWA HATUA**

Rais Samia, anaitaka Wakala wa Nishati Vijijini (REA) kuendeleza jukumu lake la kusambaza nishati vijijini, ikiwamo nishati safi ya kupikia.

Pia, anaitaka Ofisi ya Makamu wa Rais na Ofisi ya Waziri Mkuu, kuandaa na kutoa katazo la matumizi ya nishati isiyo safi kwa taasisi zinazohudumia watu zaidi ya 100 na mrejesho wa agizo hilo, taarifa yake rasmi ya utekelezaji, huo iwasilishwe ifikapo Agosti, 2024.

Aidha, anataka mkakati huo kitaifa kuchangia jitihada za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kutokana na uharibifu wa misitu, unachangiwa na shughuli za kibinadamu, hekta 469,000 za misitu zikipotea kutokana na matumizi ya mkaa na kuni.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, ambaye ni mtelekezaji mkuu wa shughuli za kiserikali, anafafanua wanatakavyowajibikia agizo hilo, kwamba:

"Mkakati huu ambao upo chini ya usimamizi wa Wizara ya Nishati na kuratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, utatakelezwa kwa gharama ya shilingi trilioni 4.6. Umezingatia miongozo ya kitaifa na kimataifa."

Hapo anaungwa mkono na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, anayesema utumiaji nishati safi ya kupika, itawasaidia wanawake na vijana kupata muda wa kufanya kazi, pia kulinda afya zao.

"Rais tunakushukuru sana kwa programu hii ya Nishati Safi ya Kupikia, ambayo itasaidia kupunguza athari kwa wanawake na vijana kwa kutumia muda mwingi kutafuta kuni na hata kupata magonjwa yanayosababishwa na moshi," anatamka Dk. Biteko.

Anaongeza; "Katika kutekeleza agizo lako (Rais) la kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia, tutahakikisha kuwa ifikapo mwaka 2034 asilimia 80 ya Watanzania, watakuwa wanatumia nishati safi ya kupikia".

Anawataja Watanzania 33,000 kila mwaka wanapatwa na magonjwa ya homa ya mapafu, kichwa, macho na saratani.

**MKAKATI ULIKOANZIA**

Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia, unaanzia hitaji la mpango jumuishi wa taifa, kukabiliana na kongezeka uharibifu wa mazingira, athari za afya, kiuchumi na kijamii kutoka matumizi ya nishati isiyo safi kupikia.

Kihistoria, tangu uhuru wa nchi mwaka 1961, haijawahi kuwa na mpango wa aina hiyo kitaifa.

Sera ya Taifa ya Nishati ya Mwaka 2015 inaeleza kungezeka matumizi ya nishati ya 'tungamotaka' na teknolojia zilizokosa ufanisi kupikia, namna za kutumia nishati za kupika na matumizi ya majiko zisizo na ufanisi, imechangia kuharibika mazingira na matatizo ya kiafya yanayohusiana na moshi.

Hapo inajenga lengo la umma kupambana, kuhamia katika

Inaendelea Uk. 12

AFYA

# Waziri Ummy aingia vitani binti apige hatua kuiona hedhi salama

**Na Yasmine Protace**



Mabinti wanafunzi wanaoangukia kundi linalopaswa kulindwa katika suala hilo. **PICHA: MTANDAO**

SUALA la hedhi salama lina maana kubwa, kusaidia jamii, ili iweze kumsaidia mwanamke kuyafikia malengo yake.

Kumekuwapo baadhi ya watoto wa kike, ambao hupitia changamoto kubwa wanapokuwa katika hali ya hedhi, wanashindwa kuhudhuria masomo kutokana na miundombinu iliyopo kutokuwa rafiki.

Tunapokuwa tunazungumzia dhana hiyo, mtu unaweza kukuta mwanafunzi anashindwa kuhudhuria masomo kutokana na kukosa vifaa vya kujisitiri wakati huo.

Vifaa hivyo vinaweza kuwa ama maji au taulo ngumu, wapo wanafunzi wanaoshindwa kuendelea na masomo kutokana na kukosa taulo ngumu na hapo wanaamua kubaki nyumbani, hadi atakapomaliza hali ya hedhi yake.

Inaelezwa, zipo baadhi ya shule hazina taulo ngumu, hivyo mtoto wa kike anapopata changamoto akiwa shuleni, anakosa msaada na kulazimika kurudi nyumbani.

Wapo baadhi ya wanafunzi wanaumwa katika hali hiyo na wanashindwa kuendelea na ratiba ya masomo kwa wakati huo.

Hapo ndipo inapopita hoja za busara zinatakiwa zitumike, ili kuwawezesha watoto wa kike wanapokuwa katika hedhi wapate mahitaji yao, ili waweze kukaa shule na kuendelea na masomo.

Ni jambo linalobaki kuwa jukumu la kijamii na wadau kuhakikisha mtoto wa kike haachwi nyuma pale anapokuwa katika hedhi.

Hivi karibuni, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu ameitaka jamii na wadau mbalimbali, kuweka mazingira rafiki kwenye suala la hedhi salama, ili mwanamke aweze kutimiza ndoto zake bila ya kikwazo chochote.

Ni sauti ya dola kuu kupitia Waziri Ummy jijini Dodoma wakati akitoa tamko kwa umma kwenye Maadhimisho ya Wiki ya Hedhi Salama, katika hatua ya uzinduzi.

"Bila hedhi salama hakuna ustawi, kwanini tuone kinyaa kuzungumza masuala ya hedhi salama?" anahoji na kuendelea: "Suala la hedhi salama hatuwezi kulikwepa ni sehemu ya kuendeleza kizazi katika jamii na taifa kwa ujumla."

Anaongeza kuwa, hedhi salama maana yake mhusika anapata elimu bila ya kikwazo, huduma katika mazingira ya vyoo, uwapo wa usiri, maji, vifaa salama na utupaji salama wa vifaa vilivyotumika.

Waziri Ummy anasema kila mwezi duniani, wanawake bilioni 1.9 wanakuwa katika kipindi cha hedhi kati ya watu bilioni saba, ambayo ni asilimia 26, wengi wakiwa ni wenye miaka 15 hadi 49.

Aidha, nchini Tanzania kwa mujibu wa takwimu za watu na makazi zilizotolewa mwaka 2022 na Ofisi ya Takwimu Taifa (NBS), kuna wanawake milioni 14.9 wana changamoto hiyo kati ya miaka 15 na 49.

"Idadi hii ni kubwa, hatuwezi kudharau mahitaji yao, hatuwezi kukaa kimya huu ni wajibu wetu kupata hedhi salama kuanzia ngazi ya kaya, taasisi mpaka jamii," anasema.

Anaongeza kuwa hedhi isiyo salama inaiathari jamii, ikiwamo mhusika kupata magonjwa kama damu chafu - UTI.

Hapo Taasisi ya Utafiti ya Magonjwa ya Binadamu (NIMR), ilifanya utafiti na asilimia 17 ya wasichana walishindwa kuhudhuria masomo kutokana na maumivu ya tumbo, kuogopa fedheha endapo wangechafuka na kukosa vifaa salama.

"Ni matumaini yangu leo tunapozindua maadhimisho ya hedhi salama itakuwa ni chachu kuwekeza katika miundombinu na vifaa ili kuwafanya kuhudhuria shuleni," anasema.

Anasema kuna mitazamo katika jamii, lakini mengine imekuwa na athari hasi zinazomnyima mwanamke haki, katika kuchangia maendeleo.

Waziri Ummy anakiri ugumu wa kuitatua akisema, masuala hayo hayawezi kumalizwa katika siku moja na serikali kupitia Wizara ya Afya, itaendelea kuwekeza ili kutekeleza afya mahususi za kuhamasisha kuondoa tabia zinazoandaa unyanyapaa kuanzia katika ngazi ya kaya.

Pia hadi sasa wizara inakamilisha mwongozo wa haja ya kuwapo hedhi salama, itakayosaidia kuondoa changamoto mbalimbali katika jamii.

Anasema serikali kwa kushirikiana na wadau, itaendelea kuweka mikakati ya kuweka utaratibu mzuri kwa msichana, kukagua upatikanaji wa mahitaji muhimu pasipo kikwazo.

Waziri anasema, kumekuwapo maadhimisho tangu mwaka 2015, lengo ni kuihabarisha jamii na kuvunja ukimya kuhusu masuala ya hedhi salama katika kuendeleza kizazi husika.

"Kila ifikapo Mei 28 kila mwaka, Tanzania inaungana na nchi zingine duniani, kuadhimisha Siku ya Hedhi Duniani, ambapo kwa Tanzania wataadhimisha wiki nzima kuanzia Mei 22 hadi 28 mwaka huu jijini Arusha," anasema.

> **"Ni matumaini yangu leo tunapozindua maadhimisho ya hedhi salama itakuwa ni chachu kuwekeza katika miundombinu na vifaa ili kuwafanya kuhudhuria shuleni," anasema.**

## Rais anavyopambana safari kufikia nishati safi kwa Watanzania 80%

**Inaendelea Uk. 11**

matumizi ya nishati nyingine kama vile gesi asilia, gesi oevu (LPG) na umeme.

Ni mkakati unaotokana na lengo la Sera ya Taifa ya Nishati ya Mwaka 2015, kuboresha maisha ya wananchi kwa matumizi ya nishati za kisasa kupikia na matamko ya kisera.

Vilevile kuna kuimarisha mabadiliko ya nishati ya kupikia kutoka kuni na mkaa, hadi nishati za kisasa; kuwezesha matumizi ya majiko na vifaa sahihi, mbadala wa kuni na mkaa.

Mkakati unashikilia Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021, inayolenga kuimarisha uhifadhi wa misitu kutunza mazingira, kupitia matumizi ya nishati

mbadala wenye gharama nafuu na zinazopatikana kirahisi kupikia;

Eneo la tatu linaungana na Sera ya Taifa ya Misitu ya Mwaka 1997, inayolenga upatikanaji endelevu wa mazao na huduma za misitu kwa kudumisha eneo la misitu nchini.

Sera ya Taifa ya Afya ya Mwaka 2007, inaelekeza kuwapo utaratibu mzuri na endelevu kuhifadhi, kutunza na kulinda mazingira kwa faida ya afya ya wanachi na vizazi vijavyo.

Kwa kuwanagalia walengwa namba moja, mama na mtoto, Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Mwanamke na Jinsia ya Mwaka 2000, inagusa kutunza mazingira kwa kumpunguzia mwanamke mzigo wa kutafuta kuni na maji, hata akashiriki vyema katika shughuli zake kijamii.

**MJADALA ULIKOTOKA 2022**

wakati akifungua Mjadala wa Taifa wa Nishati Safi ya Kupikia, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akaelekeza uandaliwe Mkakati wa Taifa wa Nishati Safi ya Kupikia utakaotoa mwelekeo wa kuhamia matumizi ya nishati safi ya kupikia ndani ya miaka 10, dira ikitaka wafikiwe asilimia 80 ya Watanzania.

Sasa, mkakati ulioundwa unainisha majukumu kadhaa, zikiwamo: Kupatikna nishati safi, nafuu, endelevu na ya uhakika kupikia kwa kuimarisha miundombinu, upatikanaji wa malighafi na kurahisisha ununuzi wa wake.

Mengine ni: Kupunguza gharama za nishati safi, vifaa na majiko sanifu ya kupikia; kuongezeka wigo wa tafiti na ubunifu wa teknolojia za nishati; Kuongezeka uwekezaji katika nishati safi yakupikia, hivyo kuchangia ukuaji uchumi.

Pia, kuwapo sera sheria, kanuni na miongozo wezeshi itakayofanikisha matumizi ya nishati safi ya kupikia; kuongezeka kwa uwezo wa watekelezaji wa miradi ya nishati safi ya kupikia.

Aidha, kuna upunguzaji wa maambukizi ya VVU na UKIMWI na kuleta usawa wa kijinsia na utawala bora katika nishati safi ya kupikia.

MAZINGIRA

# NEMC, wadau Dar walalamika wako njia panda zama kutenganisha taka

**Na Jenifer Gilla**



Huduma ya uzoaji taka ikiendelea Dar es Salaam. **PICHA: JENIFER GILLA.**

SAA 9:30 usiku, Mariam Rashid (35) anatembea akiwa na shaka mtaani kwake Vingunguti jijini Dar es Salaam, akiwa ameshikia kifurushi kikubwa cha taka.

Baada ya mwendo dakika tano anafika njia panda, anaangalia huku na kule na kujiridhisha hakuna anayemwona, kisha anatupa kifurushi na kuondoka kwa mwendo wa haraka.

Si mara ya kwanza kwa Mariam kutupa taka zilizochanganyika eneo hilo, kwani hufanya hivyo kila baada ya wiki mbili, gunia lake linapokuwa limejaa, kwa kuwa magari yaliyopewa tenda kukusanya taka majumbani hayafiki kwa wakati.

Licha ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 kuelekeza taka zote kutengenishwa majumbani, ili zikusanywe kwa utaratibu maalum kwenda kurejelezwa na kutengenezwa malighafi mengine kama mbolea, pia chakula cha samaki na kuku, imekuwa vigumu kutekelezeka.

Hiyo imesababisha mkoa wa Dar es Salaam, kuwa na taka nyingi zilizozagaa, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam (inayohudumia wilaya Ilala), inazalisha tani 4600 za taka ngumu kwa siku, kati yake asilimia 75 ni za majumbani na huishia kutupwa kwenye dampo lililoko Pugu Kinyamwezi, Wilaya ya Ilala.

Mariam anasema hafahamu chochote kuhusu maagizo ya sheria hiyo, wala hajawahi kusikia kuhusu kutenganisha taka zaidi ya kulipia tozo ya taka kwa ajili ya kuyawezesha magari kukusanya taka nyumbani kwao.

"Kwanza hiyo sheria ndio naisikia kwako mwandishi, sielewi chochote, pili hata nikitenganisha ni kazi bure, maana hayo magari yanayobeba taka yanakuja siku yanapojisikia sasa taka zinajaa ndani na hata yakija yenyewe hayatengenishi taka yanamwaga tu sehemu moja," alisema.

Wasiofahamu maagizo ya sheria kama Mariam, wako wengi; kati ya wakazi 10 wa eneo hilo waliohojiwa na Nipashe, tisa walikiri kukosa ufahamu wa sheria hiyo kuhusu kutenganisha taka majumbani.

Dorothy Paul, Mkazi wa Tabata Bonyokwa, anasema tangu amehamia katika eneo hilo kutoka mkoani Bukoba miaka mitano iliyopita hajawahi kuambiwa kuhusu kutenganisha taka na hata magari yanayokuja kuchukua hayajawapa maelekezo ya kuzitenganisha.

Anasema miaka yote aliyokaa katika eneo hilo hakujawahi kufanyika kikao na viongozi wa mtaa kuzungumzia usafi wa mazingira wala kupewa elimu ya kutenganisha taka, zaidi ya viongozi hao kupita katika nyumba zao kukusanya pesa ya kuzoa taka.

Wakati Leornard Joseph, mkazi wa Mtaa wa Butiama, Tabata anasema anafahamu kama kuna sheria ya mazingira, lakini hafahamu kama inaagiza kutenganisha taka kuanzia majumbani, na kuwatupia lawama viongozi wa serikali kuwa hawawajibiki ipasavyo katika suala hilo linatekelezeka.

Mwenyekiti wa Serikali Mtaa wa Bonyokwa, Shabani Maliyatabu, anakiri kukosekana utaratibu wa kutenganisha taka majumbani katika mtaa huo, hali inayotokana na wakazi wanaokosa elimu na msukumo huo.

Anataja jambo lingine linalokwamisha utenganishaji taka ni maslahi binafsi ya makandarasi wa kuzoa taka majumbani, wakiamini mfumo huo ukifanikiwa kuna uwezekano mkubwa wa wao kukosa tenda ya kuzoa taka majumbani.

Anaishauri serikali kuweke mfumo wa kuwabana makandarasi hao, akisema "serikali itoe tamko kama ambavyo inatoa kwenye maeneo mengine, jambo hili lijadiliwe kwenye halmashauri, majiji, kata na mitaa...."

Anaishauri serikali kuviunga mkono viwanda vya kuchakata taka ambavyo vimeonyesha mfano kama kile cha Bonyokwa ili viendelee kuwa mfano bora kwa vingine, pamoja na kuongeza viwanda kama hivyo maeneo tofauti.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Taka ya Busae, Boaz Ackim, anasema utenganishaji taka ni suala zuri, ingawa kwa upande wao linakuwa gumu kutekelezeka kwa sasa kutokana na mkataba walioingia na manispaa.

Anasema, kwa kawaida magari yanatakiwa kuzoa taka mara moja kwa wiki, hivyo kama taka zikitenganishwa majumbani watalazimika kuzoa mara tatu kwa siku, jambo ambalo ni hasara kwao kwa kuwa gharama za uendeshaji zitaongezeka.

Anashauri haja ya wao kukaa na manispaa, wajadili namna wanaweza kutekeleza mfumo huo bila wao au serikali kuathirika.

**MAONI YA WANAMAZINGIRA**

Ripoti ya Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC) ya mwaka 2017, inaonyesha kufikia mwaka 2025, taka zinazozalishwa katika jiji zinatarajiwa kuongezeka mara tatu, hivyo kunahitajika mfumo mzuri wa kusimamia utenganishwaji wa taka kuanzia majumbani, ili zirejeshwe kwa thamani na kutumika tena.

Mkuu wa Udhibiti Taka na Usafishaji Manispaa Ilala, Rajabu Ngoda, anasema wanafanya jitihada kuhakikisha mfumo wa urejelezaji taka unafanikiwa wilayani Ilala, wakianza na ujenzi wa Kituo cha Kukusanya na Kurejesha Taka cha Bonyokwa.

Kwa sasa manispaa hiyo inashirikiana na wadau wa mazingira ikiwamo HUDEFO kupitia miradi mbalimbali ya kuifikia jamii ikiwamo kuwawezesha waokota taka na kuweka mazingira rafiki ya kibiashara kwa warejesha taka.

Anataja changamoto nza kurejesha taja badio ina uhaba wa vitendea kazi, akitoa mfano hitaji la kuwapo zaidi ya magari matatu katika kila mtaa, ili kila gari lizoe aina moja au mbili kuepuka kuzichanganya sehemu moja.

Anataja faida za kurejeleza taka kutumia mfumo wa taka sifuri kuwa ni pamoja na kuongeza ajira kwa vijana, kutengeneza tishu, mbolea vyakula vya mifugo, malighafi za viwandani, na vifaa vya michezo.

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Immaculate Semesi, anasema mfumo wa 'Taka Sifuri' unafaida kubwa, ikiwamo kudhibiti taka kutupwa ovyo mitaani.

Anakiri kuwapo vikwazo katika utekelezaji wake, akinena "Ni jukumu la serikali kuu na mamlaka husika, kutoa tamko kuhusu kutumia mfumo wa taka sifuri.

"Tumeshafikisha maoni juu ya hilo sasa kilichobaki ni mamlaka kuweka nguvu katika hilo. Sisi ni wazalisha taka, lazima zirejelezwe ili kufikia taka sifuri.

"Ni uamuzi wa mamlaka za juu kutoa tamko halafu baada ya hapo sisi tutafuatilia na kuingia mtaani kutoa elimu kuhusu umuhimu wake, tunatakiwa kuwa na gari angalau lenye sehemu mbili au zaidi ya kuweka taka zilizo tenganishwa..."

Analalamika kuna sheria ya mazingira, ambayo utekelezaji wake bado unasuasua, akitamani kila idara na taasisi kisekta, kuwa na kipengele cha mazingira kisheria, iwajibike nayo.

**WADAU WAZUNGUMZA**

Mkurugenzi wa Taasisi ya Human Dignity and Environmental Care Foundation (HUDEFO), Sarah Pima, anasisitiza kutolewa elimu kwa viongozi wa mitaa, ili wakaitoe kwa wananchi waone umuhimu wa kutenganisha taka majumbani mwao.

Hilo anashauri kuendana na haja ya kuwapo mapipa ya kutenganishwa mitaa, ili magari yawe yanakusanya katika mapipa hayo, kwa kuwa magari yamekuwa na mazoea ya kuchelewa, hata wananchi wanatupa taka mitaani.

Anashauri kuwapo vituo vya kukusanya taka hizo kila wilaya na kuziuza kwa wafanyabiashara wanaorejesha taka, tofauti na sasa kituo tu wilayani Ilala.

Alisema pia wamekuwa wakitoa elimu kwa pamoja waokota taka hasa chupa za plastiki juu ya njia salama za kazi hiyo pamoja na kuwapa vitendea kazi na eluimu ya biashara ili wafanye kazi yenye faida na kujiletea maendeleo kupitia kazi hiyo.

Anasema kupitia mfumo huo, HUDEFO wamepata mafanikio katika utenganishaji taka katika maeneo ya Dar es Salaam na Asilimia 95 ni wanaoioshi katika jamii ya kipato cha chini, wamekubali utenganishaji wa taka.

Anord Shoko, Mkurugenzi wa Taasisi ya LIMA inayojishughulisha na kutengeneza chakula cha kuku na samaki kwa kutumia taka za majumbani, anataja haja ya serikali kuongeza nguvu kuweka vituo vya kuuzaa taka zilizotengenishwa.

Anasema, kuna changamoto kuu wanayokutana nayo, ni kupata taka hizo na wamekuwa wakijitahidi kuzinunua majumbani.

"Kuna wakati tunahitaji tani moja ya taka lakini upatikanaji wake ni wa shida, hatuwezi kuzipata kwa haraka kwa mara moja mpaka tuzunguke sana na kuwatumia watu, lakini kama kukiwa na kituo cha kutenganisha taka wilaya hii ingeturahisishia sana," anasema.

AFYA

## MADHARA YAIKURUPUSHA TMDA...

# Simulizi maduka dawa kuuza bidhaa zilizoishia muda mtaani

## •Serikali Mtaa yanunua kesi, bidhaa Mil. dukani



Dawa zikiwa dukani. Picha nyingine ni baadhi ya dawa. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Shaban Njia, KAHAMA.**

KUKOSEKANA elimu ya kutambua bidhaa ya dawa za binadamu zilizokwisha muda wake wa matumizi hasa za kumeza, kunalalamikiwa kusababisha watumiaji kuwa hatarini kiafya na kupata ugonjwa sugu, wahanga wakubwa ni wanawake na watoto.

Dawa zinazotolewa kwa njia ya sindano pia si salama kuzitumia baada ya kuisha muda kwani zinaweza kusababisha madhara makubwa kwani vijidudu kama fangasi na bakteria, huweza kuota kwenye dawa hizo zenye asili ya majimaji na kuleta madhara makubwa zaidi endapo wataingia mwilini.

Kutokana na ukubwa wa tatizo hilo, Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), imekuwa ikifanya ukaguzi wa kila mara katika maduka ya dawa za binadamu, lengo ni kudhibiti dawa zilizokwisha muda wake wa matumizi zisiendelee kusambaa mitaani na wanaobainika kuuza, wanachukuliwa hatua za kisheria.

Katika Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga, ,wakazi walikuwa wakilalamika kuuziwa dawa katika moja ya duka la dawa lakini walikuwa hawaponi magonjwa wanayoumwa, hatua iliyowafanya kupaza sauti mpaka TMDA ilipofika na kubaini kuwepo dawa zilizokwisha muda wa matumizi.

Mkaguzi wa TMDA, Venancy Burushi anasema wamekuwa wakifanya ukaguzi wa maduka ya dawa mara kwa mara ili kupambana na dawa zilizokwisha muda zisiendelee kutumiwa kwani zinamadhara makubwa na zinasababisha mpaka kifo.

Anasema, kuuza dawa zilizokwisha muda wake wa matumizi ni kwenda kinyume na Kifungu Namba 76 cha Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba na kuna baadhi ya dawa kama kundo la antibaiotiki, hugeuka kila bada aya muda wake wa matumizi kuisha na kusababisha matatizo kwenye figo.

Burushi anasema, dawa mara nyingi hubaki na uimara wake inapotunzwa sehemu salama hasa kwenye ukavu, yenye ubaridi baridi na mbali na joto au mwanga wa jua, zinapotunzwa nje ya mazingira hayo zinaharibika na kutengeneza sumu ndio sababu yakuwa wanakagua mara kwa mara maduka.

Burushi anasimulia atika mtaa wa Mwine Manispaa ya Kahama wamemkamata mfanyabiashara (jina tunalo) akiuza dawa za binadamu zilizokwisha muda wa matumizi na kujipatia fedha pasipo halali, huku wananchi wakilalamika kutopona wakitumia dawa hizo.

Anazitaja dawa hizo kuwa ni pamoja na Tinidazole, Good Morning na Cafenol, zilizokuwa zimekwisha muda wake wa matumizi, lakini mmiliki wa duka akaendelea kuwauzia wananchi, huku akijua ni kosa kisheria.

"Dawa zote hizi tulizozikamata zimeghushiwa muda wa matumizi, ambazo zipo zinaoonesha zimekwisha matumizi Desemba mwaka 2023 na zingine zimeongezwa muda wa matumizi na ambazo zinatakiwa kwsha Septemba 24 mwaka huu, ila zimeongezwa muda hadi Oktoba Mwaka 2025," anasimulia Burushi.

Meneja wa TMDA Kanda ya Ziwa Magharibi Dk. Edgar Mahundi, anasema dawa zote zilizokamatwa zimethaminishwa na gharama yake ni Sh. Milioni tano na kama zingeuzwa kwa binadamu zingeleta madhara makubwa, ikiwamo kupata tatizo la usugu wa dawa mwilini.

Aidha, anasema watamfungulia mtuhimiwa waliomkamata, mmiliki wa duka hilo, kwa kukiuka sheria za uuzaji dawa za binadamu, kwani kitendo cha kuuza dawa bandia au zilizokwisha muda wake ni kinyume cha sheria, akisisitiza madhara yalivyo, mtumiaji anaweza kupata madhara usugu wa dawa mwili, kupooza viungo au kifo.

Mahundi anatoa onyo kali kwa wafanyabiashara wa dawa za binadamu kuacha udanganyifu kwa kucheza na maisha ya binadamu kwa kuuza dawa zilizokwisha matumizi na TMDA haitawavumia.

Hapo anaahidi atahakikisha wanafikishwa mahakamani wote watakaobainika, akiwataka wananchi kuangalia muda wa matumizi wa bidhaa wanayonunua.

**MAONI YA WANANCHI**

Mkazi wa Mtaa wa Mwime Hassan Said anasema, kutokuwa na elimu ya kutambua bidhaa zilizokwisha muda wake wa matumizi hasa dawa za binadamu zinasababisha kuwa na usugu wa maradhi wanayoumwa mara kwa mara na wamekuwa wakigundua pale wanapofika vituo vya afya na hospitali na kuonyesha dawa walizotumia.

Anasema, baadhi yao wanalazimika kukimbilia kwa waganga wa jadi kupata matibabu kiasili, huku wakiwa hawatambui kuwa wanahatarisha usalama wa maisha yao kwani ugonjwa wa malaria na hautibiwi kwa wakunga jadi, hali inayowasababisha wanatumia dawa za kizungu lakini hawaponi wala kupata unafuu wowote.

Saidi anasema, wiki mbili zilizopita ndugu yake alidhurika kwa kupewa dawa katika maduka mtaani na ilipofuatiliwa, muuzaji katika duka la dawa alikuwa mkali, lililowaumiza na kutoa taarifa kwa

> **"Dawa zote hizi tulizozikamata zimeghushiwa muda wa matumizi, ambazo zipo zinaoonesha zimekwisha matumizi Desemba mwaka 2023 na zingine zimeongezwa muda wa matumizi na ambazo zinatakiwa kwsha Septemba 24 mwaka huu, ila zimeongezwa muda hadi Oktoba Mwaka 2025," anasimulia Burushi.**

Mwenyekiti wa Serikali Mtaa, kwa hatua zaidi.

Aika Samweli, anasimulia "Mwezi wa Kwanza mwaka huu (Januari), niliugua sana na mara baada ya kupima nilibainika kuuzwa malaria na UTI. Nilitumia dawa ndani ya wiki nzima sikuweza kupata unafuu wowote..."

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Mwime, Dogo Mhenziwa, anasema ofisi yake imekuwa ikipokea malalamiko ya wananchi kuuziwa dawa zilizokwisha muda na wanazitambua, kwa malalamiko ya watu kutopata nafuu au kupona.Sasa anaiomba serikali kutoa elimu ya namna ya kuzifahamu bidhaa zilizokwisha muda wake wa matumizi ili kuondoa madhara yasiyo na ulazima.

Anasema, wamekuwa wakishuhudia makundi maalumu mbalimbali yakipewa elimu ya kutambua bidhaa kama fedha bandia, hivyo basi nguvu kama hiyo ifikie wananchi kwa kuelimishwa na kutambua bidhaa feki kupitia vyombo vya habari na mikutano ya hadhara inayofanyika.

Mhenziwa anaeleza, mtaani kwake kunamiliki wa duka mmoja amekuwa akikamatwa na polisi mara kwa mara kwa tuhuma za kuuza dawa zilizokwisha muda wake wa matumizi lakini amekuwa akifika kituo na kuachia na ninadhani ni kwa sababu hata polisi hawana elimu ya kuzitambua bidhaa hizo.





## TRA yajivunia makusanyo kupaa miaka 3 ya Samia

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) Mkoa wa Dodoma imeongeza wastani wa ukusanyaji kodi kutoka Sh.bilioni 15.19 hadi Sh.bilioni 18. 71 katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi kuhusu mafanikio ya mamlaka hiyo jijini hapa, Meneja wa TRA, Mwita Ayubu, alisema mafanikio hayo ya makusanyo yametokana na uboreshaji wa uhusiano kati yao na walipakodi.

Alisema kuwa mwaka 2021 Mkoa wa Dodoma ulikuwa na wafanyabiashara 3,812 wanaotumia mashine ya EFD, hivi sasa wameongezeka na kufikia 9,367 ikiwa ni ongezeko la wafanyabiashara 5,555.

"Mengine yaliyowezesha kupanda kwa kiasi hicho cha fedha cha ukusanyaji ni ongezeko la uwekezaji na ukuaji wa shughuli za kiuchumi ikiwamo uzalishaji viwanda na sekta za ujenzi na usafirishaji na uhamasishaji kwa kupitia elimu kwa mlipakodi," alisema.

Alibainisha kuwa pia ongezeko la matumizi ya mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika usimamizi wa kodi kutoka kwa wananchi kwa kulipa kodi kwa hiari, kuongezeka kwa hamasa ya ulipaji kodi kutoka kwa wananchi kwa kuona matumizi sahihi ya kodi wanazolipa.

Hivyo, aliwasisitiza wafanyabiashara kutumia mashine za EFD kutokana na kuwapo kwa faida kama vile uboreshaji wa kumbukumbu za biashara kwa njia za elektroniki ambayo ni salama na ya kuaminika.

Hata hivyo, alisema mamlaka hiyo inakabiliana na tatizo la kuongezeka kwa wimbi la matumizi ya stempu za kielektroniki za kughushi kwa walipakodi, hali inayosababisha upotevu mkubwa wa mapato.

# RC ageuka mbogo ujenzi wa hospitali ya rufani kusimama

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, ameamuru kuitwa kwa mkandarasi wa jengo la ghorofa la Hospitali ya Rufani Mkoa wa Singida ili kueleza sababu za ujenzi kusimama tangu mwaka 2022.

Amri hiyo aliitoa jana baada ya kutembelea hospitali hiyo kwa lengo la kukagua miradi inayojengwa akiwa ameambatana na Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Singida, Martha Mlata na Katibu wake, Lucy Boniface.

Katika ukaguzi huo, mkuu huyo wa mkoa, alibaini ujenzi wa jengo la ghorofa tatu lililokuwa linajengwa na mkandarasi MCB Co. Limited ambaye ni Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya ujenzi umesimama kwa zaidi ya miaka miwili sasa huku Sh. bilioni 6 zilizotolewa na serikali zikiwa hazijatumika.

"Kwa nini kila mkataba mnavunja wakati kuvunja mkataba ni gharama, sasa mwiteni huyo mkandarasi tuje tuongee naye tuangalie namna atakavyoweza kumalizia ujenzi uliobaki maana kusema unampa mkandarasi mwingine ni gharama, " alisema.

Dendego, alisema ni lazima jitihada zifanyike ujenzi uanze mapema ili kunusuru fedha hizo Sh.bilioni 6 kurudishwa serikalini mwaka mpya utakapoanza Julai 1, mwaka huu.

Kuhusu watumishi wanaojitolea kwa muda mrefu bila kupata ajira, aliwaagiza viongozi wa hospitali hiyo kumpatia orodha ili aweze kuwasaidia waajiriwe.

Kwa upande wake Mlata, aliwasisitiza watumishi wa hospitali hiyo kuendelea kuchapa kazi kwa bidii kwa sababu serikali inawajali na itaendelea kutatua changamoto zinazowakabili kwa muda mwafaka.

Naye Boniface aliwataka watumishi hao watambue kuwa kazi wanayoifanya ni ya wito, hivyo wasikate tamaa kwani kumhudumia mtu hadi aridhike ni kazi ngumu.

Awali Kaimu Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Davis Mwasota, alisema jengo hilo ujenzi wake ulianza mwaka 2014 na kusimama 2022 baada ya kuvunja mkataba kutokana na uwezo mdogo wa mkandarasi.

Dk. Mwasota, alisema mradi huo ambao upo asilimia 78 ya ujenzi kwa sakafu ya chini na asilimia 36 sakafu ya pili hadi sasa umetumia Sh.bilioni 3.6 na kwamba kiasi cha Sh. bilioni 2.3 hakijatuma.

Alisema katika mwaka wa fedha wa 2023/2024 Sh.bilioni 4 zilitengwa kwa ajili ya ujenzi, lakini hazijaombwa kwa kuwa mradi umesimama.

Alisema Wizara ya Afya inakamilisha mkataba na mshauri elekezi baada ya kubaini wakati wa utekelezaji wa mradi kulikuwa na changamoto.



Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwani Kikwete (katikati), akijadiliana jambo na Naibu Waziri wa Ujenzi, Godfrey Kasekenya (kushoto) pamoja na Naibu Waziri wa Fedha, Hamad Chande, Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Waziri Mhagama azibana taasisi za umma

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu, Jenista Mhagama, ameziagiza taasisi za umma kufanya tathmini ya awali ya hali ya utekelezaji wa mfumo wa ufuatiliaji na kuwasilisha ofisini kwake kabla Julai, 15 mwaka huu.

Mhagama alitoa maagizo hayo juzi jijini hapa wakati wa uzinduzi wa nyaraka za msingi za ufuatiliaji na tathmini nchini na utiaji sahihi mikataba ya makubaliano katika kuimarisha shughuli hizo.

Alisema kuzinduliwa kwa nyaraka hizo kutasaidia kuongeza ufanisi katika ufuatiliaji wa tathmini na kuhimiza matumizi ya matokeo yake katika kufanya maamuzi na kuboresha utekelezaji na utendaji katika ngazi zote.

"Katika kutekeleza hili naelekeza taasisi za umma kuandaa taarifa ya utekelezaji wa tathmini zote zilizofanyika kwa mwaka wa fedha 2023/24 na zinazotarajiwa kufanyika kwa mwaka wa fedha 2024/25 ili ofisi yangu iweze kuandaa mpango wa tathmini wa mwaka 2024/25 na kufuatilia utekelezaji wake," alisisitiza.

Vilevile alielekeza wakuu wa taasisi za umma kufanya tathmini ya awali ya hali ya utekelezaji wa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini katika taasisi zao.

Maelekezo mengine ni pamoja na kuandaa mpango wa ufuatiliaji kwa kuonesha maeneo na kazi zote zitakazofuatiliwa kila siku kulingana na mpango kazi wa taasisi na mipango ya utekelezaji wa afua mbalimbali, kuandaa mpango wa tathmini kwa kuonesha tathmini za afua za maendeleo zitakazofanyika katika kipindi husika.

Mhagama, alielekeza kuandaliwa kwa moduli za utendaji zinazojumuisha viashiria muhimu vya kupima utendaji wa taasisi, kuteua wataalamu kutoka idara na vitengo vyote vya taasisi husika.

Alisema wataalamu hao watashirikiana na idara/kitengo cha U&T katika utekelezaji wa mwongozo huo.

Waziri huyo aliwasisitiza makatibu wakuu, watendaji wakuu, makatibu tawala wa mikoa na wakurugenzi wa mamlaka za serikali za mitaa na wakurugenzi wa vitengo vya U$T katika taasisi za umma kuendelea kuimarisha vitengo vya ufuatiliaji na tathmini.

Awali Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu, Dk. Jim Yonazi, alisema mwongozo uliozinduliwa na nyaraka za ufuatiliaji na tathmini zinalenga kuziongoza taasisi za umma namna ya kutekeleza majukumu ya ufuatiliaji na tathmini.

"Mwongozo huu umeainisha hatua za kufuata katika ufuatiliaji, ufanyaji wa tathmini, maandalizi ya viashiria na kupima utendaji wa shughuli za serikali.

Mkuu wa Taasisi ya Uongozi, Kadari Singo, alisema upo umuhimu wa kuendelea kusimamia vitengo vya ufuatiliaji na tathmini katika wizara na taasisi ili kusaidia kuleta matokeo yanayokusudiwa na kuongeza ufanisi kutekeleza majukumu ya kila siku.





# Pareto hatarini kuporomoka kimataifa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

LICHA ya uzalishaji wa pareto kuongezeka nchini, ubora wake umeporomoka kutokana na wakulima kuzalisha bila kufuata kanuni za kilimo bora na kutishia soko la kimataifa, imeelezwa.

Ofisa Kilimo wa Kampuni ya Pareto Tanzania (PCT), Mussa Malubalo aliyasema hayo juzi wakati akitoa zawadi kwa wakulima waliofanya vizuri kwenye uzalishaji wa zao hilo katika Wilaya ya Mbeya ambayo ndiyo inaongoza kwa uzalishaji huo katika Mkoa wa Mbeya.

Wakulima waliopatiwa zawadi ni wale ambao walifuata kanuni bora za uzalishaji wa pareto ikiwamo kufanya palizi vizuri na kwa wakati na kuchuma maua yaliyokomaa vizuri.

Malubalo, alitaja sababu ya kuporomoka kwa ubora wa pareto kuwa ni pamoja na baadhi ya wakulima kuchuma maua ambayo hayajakomaa, kukausha maua kwa kuanika chini na kuchanganyika na uchafu.

"Kuna shida kubwa kwenye kilimo cha zao hili kwa sasa ubora umeshuka kwa kiwango kikubwa sana, sisi tumekuwa tukitatua kero ikiwamo kuwasaidia kujenga vikaushio vya kisasa, kugawa mbegu bora na motisha kwa wakulima wanaofanya vizuri," alisema Malubalo.

Alisema katika msimu huu wa kilimo, wanakusudia kuongeza ununuzi wa zao hilo kutoka tani 2,000 za msimu uliopita mpaka tani 2,500 na kununua kilo kwa Sh. 3,500.

Alisema pia wanakusudia kujenga vikaushio vya kisasa 200 ili kufikisha 521. Kabla ya msimu huu kuanza, walijenga vikaushio 321 katika maeneo mbalimbali nchini ambako zao hilo linazalishwa.

Mwenyekiti wa Bodi ya Pareto nchini, Lucas Kiayo, alisema kwa mara ya kwanza msimu uliopita uzalishaji wa zao hilo ulifikia zaidi ya tani 4,000 kiwango ambacho hakijawahi kufikiwa tangu nchi ilipopata uhuru.

Kiayo, alisema ongezeko hilo lilitokana na elimu ambayo wakulima wamekuwa wakipatiwa pamoja na kuongezeka kwa maeneo ya uzalishaji hasa katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

Aliwataka wataalamu kuendelea kutoa elimu kwa wakulima ili waboreshe kilimo cha zao hilo kwa kuzalisha pareto inayokidhi mahitaji ya soko la kimataifa ikiwamo yenye kiwango sahihi cha sumu.

"Wakati huu ambao uzalishaji unaongezeka ni vema tukaweza nguvu kubwa kwenye ubora wa zao hili ili kuhakikisha tunakidhi mahitaji ya soko la kimataifa, wataalamu wetu wa kilimo wajitahidi kutoa elimu kwa wakulima," alisema Kiayo.

Baadhi ya wakulima bora wa zao hilo, waliishukuru serikali kwa kuendelea kuwawekea mazingira rafiki ya uzalishaji na kuuza kwa bei nzuri ambayo inawapatia faida.

Mmoja wa wakulima hao, Gideon Mapunda, alisema PCT imewasaidia kuzalisha kwa ubora na kubadilisha maisha kwa kujenga nyumba bora na tofauti na miaka ya nyuma.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa, alisema serikali itaanza kuzibana kampuni zinazojihusisha na ununuzi wa pareto mbichi hali inayosababisha kupungua kwa ubora wa zao hilo na kuharibu soko la kimataifa..



Balozi wa China nchini Tanzania, Chen Mingjian, akizungumza wakati wa mdahalo wa vijana wa China na Tanzania, katika Chuo Kikuu cha Dar as Salaam jana. Kulia ni Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu), Patrobas Katambi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wanunuzi wawanyonya wakulima parachichi

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

SERIKALI wilayani hapa Mkoa wa Njomba imepiga marufuku wanunuzi wa parachichi matunda daraja la pili kwa bei ya chini kwa kuwanyonya wakulima.

Amri hiyo ilitolewa juzi na Mkuu wa Wilaya Njombe, Kissa Kasongwa baada ya kupata taarifa kuwa baadhi ya wafanyabiashara wananunua kilo moja ya matunda hayo kwa bei ya Sh. 200 ambayo haina faida kwa wakulima zaidi ya kuwadidimiza.

Akizungumza na wakulima wa zao hilo wa Halmashauri ya Mji wa Njombe, alisema wanunuzi hao wanatakiwa kupata kibali maalumu kutoka serikalini.

"Hataruhusu mnunuzi yeyote wa parachichi kununua parachichi daraja la pili (reject) pasipo kibali kutoka serikalini. Kumekuwa na wanunuzi ambao wananunua parachichi daraja la pili kwa kujipangia bei wenyewe wakiwatisha wakulima kuwa zitaoza au zitawafia," alisema Kasongwa.

Alisema hayuko tayari kuona wakulima wa parachichi wanaingia kwenye mkwamo mkubwa wa soko la tunda hilo ilihali wametumia gharama kubwa katika uzalishaji.

Aliwaagiza maofisa ushirika wilayani hapa kuanzisha ushirika wa umoja wa wakulima wa parachichi (AMCOS) kutokana na mwongozo wa Wizara ya Kilimo.

"Marufuku uvunaji na ununuzi wa parachichi kwa kutumia mifuko (kiroba) hii sio nzuri inahatarisha ubora wa zao hili katika soko la kimataifa," alisema Kasongwa.

Baadhi ya wakulima akiwamo Atukuzwe Mwendamseke, alisema hali imekuwa mbaya kutokana na kukosa njia mbadala ya kukabiliana na changamoto za maisha na kujikuta wanauza parachichi kwa bei ndogo.

Mkuu wa Idara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi kutoka Halmashauri ya Mji wa Njombe Thadei Luoga, alisema anakwenda kusimamia maelekezo hayo ili kusaidia mkulima kuendelea kuzalisha zaidi. Ofisa Vipimo Mkoa wa Njombe, Shaban Kingu, kwa niaba ya meneja wa Vipimo, alipiga marufuku kutumia kipimo kingine tofauti na mzani kwa zao la aina yoyote mkoani humo.

Mmoja wa wanunuzi wa parachichi mkoani humo, Erasto Ngole, licha ya kukiri kuhusika kwenye baadhi ya changamoto, aliwataka wakulima kuzingatia ubora katika matunda yao ili kukabiliana na kikwazo katika soko la kimataifa.

# Walia kukosa maji, kisa barabara

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKAZI wa Kata ya Ilemi Halmashauri ya Jiji la Mbeya, wamekosa huduma ya majisafi kwa zaidi ya miezi mitano kutokana na miundombinu ya maji kukatwa na mkandarasi anayejenga barabara ya Ilemi hadi Machinjioni kwa kiwango cha lami.

Wakazi hao walitoa malalamiko hayo juzi kwenye mkutano wa hadhara uliowashirikisha viongozi na watendaji wa halmashauri hiyo kusikiliza kero na kuzitatua.

Mmoja wa wakazi hao, Angelo Magamo, alisema mkandarasi huyo wakati anaanza kujenga barabara hiyo alikata mabomba na kuahidi kuruhusu miundombinu hiyo kurejeshwa baada ya kukalimisha ujenzi wa barabara hiyo.

Alisema mpaka sasa wanaelekea mwezi wa tano ujenzi wa barabara umekwama na wao kuendelea kukosa maji.

"Tunapata shida sana, huyu mkandarasi aliishia kumwaga vifusi na kusababisha tushindwe kupita kwenye hii barabara, sasa hilo siyo tatizo sana kwetu bali kukosa maji ndio tunaomba mtusaidie," alisema Magamo.

Meya wa Jiji hilo, Sheikh DorMohamed Issa, alisema mwenendo wa mkandarasi huyo hauridhishi licha ya kumlipa zaidi ya Sh. bilioni 2.5 kwa ajili ya ujenzi huo.

Issa, alisema mkandarasi huyo alitakiwa kukamilisha kazi hiyo ndani ya mwaka mmoja na kwamba baada ya kufuatiliwa ameahidi mwisho ni Oktoba mwaka huu.

Aliwataka wakazi hao kuwa wavumilivu wakati ujenzi huo ukiendelea.

Barabara hiyo ni miongoni mwa miradi inayotekelezwa kupitia Programu ya Kuboresha Majiji (TACTIC).

**Mmoja wa wakazi hao, Angelo Magamo, alisema mkandarasi huyo wakati anaanza kujenga barabara hiyo alikata mabomba na kuahidi kuruhusu miundombinu hiyo kurejeshwa baada ya kukalimisha ujenzi wa barabara hiyo.**



## ‘Sekta ya viwanda haifanyi vizuri’

**Na Faustine Feliciane**

SHIRIKISHO la Viwanda Tanzania (CTI) limesema sekta ya viwanda nchini haifanyi vizuri, hivyo juhudi zinahitajika kuongeza ufanisi na kufikia malengo ya kuimarisha uchumi wa viwanda.

Katika hafla ya kutia saini makubaliano ya ushirikiano kati ya CTI na Tume ya Ushindani (FCC) jana jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa shirikisho hilo, Leodgar Tenga, alisema juhudi zaidi zinatakiwa kuvuta wawekezaji na kuongeza tija kwenye viwanda.

Alisema makubaliano ya ushirikiano waliyoingia na FCC yatasaidia kuboresha utendaji wa taasisi hizo.

“Viwanda havifanyi vizuri kama tunavyotaka, juhudi kama hizi zitatupeleka mbele zaidi, lazima tushirikiane kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji na ufanyaji biashara nchini,” alisema Tenga.

Mkurugenzi Mkuu wa FCC, William Urio, alisema makubaliano hayo pia yanalenga kuangalia namna bora ya kubadilishana taarifa ili kufikia malengo ya serikali ya kukuza uchumi wa viwanda.

“Makubaliano haya ya kihistoria pia yatasaidia kutekeleza sheria mbili ambazo zinatugusa sote, sisi FCC na wenzetu wa CTI. Sheria hizi ni Sheria ya Ushindani na Sheria ya Alama za Bidhaa, tunataka kuona ushindani wa kibiashara hasa kwenye viwanda unakua zaidi na pia kusaidiana kutekeleza sheria hii ya alama za bidhaa,” alisema.

Urio alisema kuwa ili kuunga mkono juhudi za serikali katika kuvutia wawekezaji na kuweka mazingira mazuri ya biashara, taasisi hizo ni lazima zizingatie sheria na kuzisimamia.

“Bila ushindani hakuna maendeleo ya viwanda, tunahitaji ushindani sahihi na wa halali, hakuna upangaji bei wa hujuma kwa wenye viwanda na pia kuzingatia sheria kwenye masuala ya zabuni,” alisema.

**Alisema makubaliano ya ushirikiano waliyoingia na FCC yatasaidia kuboresha utendaji wa taasisi hizo.**

# Naibu Spika azipasha asasi za kiraia kuacha ubinafsi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mgeni Hassan Juma amezitaka asasi za kiraia kuacha ubinafsi na kujenga imani kwa jamii kwa kusaidia kuwainua wanawake katika uongozi na serikali.

Rai hiyo aliitoa mwanzo mwa wiki hii wakati akifunga Mkutano wa Jukwaa la Kitaifa la Kimkakati na Midahalo ya Kiuchechemuzi kwa asasi hizo lililofanyika visiwani hapa.

Alisema bado kuna tatizo kubwa la wanawake kushika nafasi za uongozi, hivyo asasi hizo zina jukumu la kuwahamasisha wanawake kugombea uongozi hasa katika kipindi hiki cha kuelekea Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025.

Alisema baadhi ya asasi hizo zinashindwa kutekeleza wajibu wao, licha ya kusajiliwa kisheria na kwamba zinaomba miradi kutoka kwa wafadhili kwa lengo la kujipatia fedha kwa maslahi binafsi badala ya kusaidia jamii.

“Zipo asasi za kiraia zilizosajiliwa zaidi ya 200, lakini zinazofanya kazi vizuri ni chache tu, nyingi ofisi zao zipo mifukoni mwa viongozi wa asasi hizo,” alisema Naibu Spika huyo.

Alisema uhusiano kati ya serikali na asasi hizo unajenga taifa imara katika kuleta maendeleo nchini kwa maslahi ya wananchi. Mkurugenzi wa Wanawake wenye Ulemavu Zanzibar, Bakari Hamad, alisema jumuiya yake ipo tayari kutengeneza mazingira wezeshaji ya wadau ili kuimarisha asasi hizo kutekeleza wajibu kwa kufuata misingi ya kisera.

Akiwasilisha mapendekezo kwa washiriki wa mkutano huo, Mtaribu wa Mradi wa Uraia Wetu unaotekelezwa na Jumuiya ya Wanawake wenye Ulemavu (JUWAUZA), Selemani Baitani, alisema kuna changamoto zinazozikabili asasi hizo.

Bataini alitoa mfano kuwa ni kufuata sheria za kuchangia mifuko ya hifadhi ya jamii baada ya asasi kushiriki katika harakati za uchaguzi mkuu nchini.

Alisema asasi hizo zinahitaji mazingara yalioboreshwa katika masuala ya kodi ili kuchangia zaidi maendeleo ya nchi.

Alisema asasi hizo hazina mwakilishi katika baraza hilo la wawalishi na kwamba wanahitaji kuwa naye kama ilivyo kwa Bunge la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.



Waziri wa Afya Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui akizungumza katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani nje ya mji wa Zanzibar jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Miundombinu yaboreshwa Mji Mkongwe

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema juhudi za kuimarisha Mji Mkogwe kwa kuboresha miundombinu ya maji safi na salama, barabara na umeme ili uwe na sifa za kimataifa.

Hayo yalisemwa jana katika Kikao cha Baraza la Wawakilishi na Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Mudrik Ramadhan Soraga wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Kojani, Hassan Hamad Omar.

Mwakilishi huyo alitaka kujua mikakati ya kuimarisha mji huo wa Zanzibar kutambuliwa kuwa ni miongoni mwa iliyopo katika urithi wa kimataifa ikoje.

Soraga alisema kusema kuwa kazi kubwa inayofanyika kwa sasa ni kuubadilisha mji huo kuwa na hadhi ya kimataifa zaidi na kuendelea kutambuliwa na taasisi za kimataifa.

Kwa mujibu wa Soraga, Kampuni ya National Energy ya Oman imechukua jukumu la kusambaza miundombinu ya majisafi na salama katika mji huo.

Alisema mradi wa BIG-Z unatekelezwa na Benki ya Dunia (WB) katika mjio huo kwa ajili ya kuimarisha miundombinu ya barabara.

“Hiyo ndiyo mikakati yetu katika kuimarisha mji mkongwe wa Zanzibar kuona kwamba mji huo unaendelea kuwa na sifa na hadhi ya mji iliopo katika urithi wa kimataifa,” alisema.

Alisema mji huo bado upo salama na hakuna tishio la kuondolewa katika mji iliyopo katika urithi wa dunia.

Soraga, alisema mji huo umebeba historia ya mambo mengi, ikiwamo majengo ya kale ambayo yamejengwa na watawala mbalimbali na kuwa kivutio kwa watalii.

“Mheshimiwa Spika Mji Mkongwe wa Zanzibar ni muhimu katika kutangaza utalii wa Zanzibar na mambo ya kale, tutahakikisha unaimarishwa katika miundombinu yake yote,” alisisitiza.

mwisho.

**Hayo yalisemwa jana katika Kikao cha Baraza la Wawakilishi na Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Mudrik Ramadhan Soraga wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Kojani, Hassan Hamad Omar.**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**THE REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT**
**CAP. 117 R.E 2002**
**CHANGE OF NAME BY DEED POLL**

By this deed I the undersigned ASHA MOHAMED NCHINCHI of P.O.Box DAR ES SALAAM do hereby absolutely renounce and abandon the use of my said name ASHA MOHAMED and in pursuance of such change of name as aforesaid I hereby declare that I will at all time thereafter in all records deeds and all occasions whatsoever use and sign the said name of ASHA MOHAMED NCHICNHI as my name in lieu of my said former name of ASHA MOHAMED renounced as aforesaid.

And I HEREBY expressly authorize and require all and every person whatsoever at all times after the date hereof to design designate, describe and address me by the adopted name of ASHA MOHAMED NCHINCHI

In WITNESS WHERE OF I have unto set my hand at Dar es salaam and I here on substitute my old name of ASHA MOHAMED by my new name of ASHA MOHAMED NCHINCHI

SIGNED and DELIVERED by the said ........ who is known to
Me personally/identified by to me by ......
The latter being known to me personally
In my presence this ...22... day of FEB 2024

DEPONENT

Name ........
Designation ........
Signature ........
Date ........



---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO BOMA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**MKOA WA MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na...26/2024**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: MOHAMED SALUM LUSOGO wa MOROGORO**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOLETWA NA HUSSEIN MOHAMED LUSOGO**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo Tarehe 18 Mwezi 6 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
- Endapo kuna yoyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia

Imetolewa leo Tarehe 4 mwezi 6 mwaka 2024

HAKIMU

---

**IN THE DISTRICT COURT OF KYELA**
**AT KYELA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 12402/2024**
**IN THE MATTER OF THE ESTSTAE OF THE LATE GWANDUMI ANDENDEKISYE MWAIPUNGU**
**AND**
**In the matter of Application for letters of Administration by**
**HAGAI GWANDUMI MWAIPINGU......PETITIONER**

**GENERAL CITATION (RULE 75)**

All persons claiming to have interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceeding if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 04th day of july 2024.

Dated at kyela this 31st day of May, 2024

DISTRICT COURT KYELA TANZANIA

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
KYELA

---

**IN THE DISTRICT COURT OF KYELA**
**AT KYELA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 12163/2024**
**IN THE MATTER OF THE ESTSTAE OF THE LATE LABISONI ALIJULA MWAKALILE**
**AND**
**In the matter of Application for letters of Administration by**
**MARIAMU MUNDERA LABISONI.........PETITIONER**

**GENERAL CITATION (RULE 75)**

All persons claiming to have interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceeding if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 02nd day of July 2024.

Dated at kyela this 31st day of May, 2024

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GODSON ELIREHEMA MKUMBWA**

ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NO YA USAJILI T357 BGJ RAV 4 YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI

**PHQ/ARU/ARU/ 16979/2024.**

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**IRENE IBRAHIM NTAGALUGWA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S5163-0022, KWEMA MODERN SECONDARY SCHOOL** mwaka **2017.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA:PHQ/KIG/KAS/1558/2024**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**JOSEPH PAULO ZIZIMA**

anatangaza kupotea kwa kadi ya Bajaji yenye namba za usajili MC847CMR aina ya BAJAJ REAR, Chassis No. MD2A25BY4KWB37423, Engine No. AZZWKB02566. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

TAARIFA YA POLISI:

**DOD/DOD/RB/9771/2023**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 11085 of 2024**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE SAMWEL LAZARO CHIMELA DECEASED OF MPUNGUZI, DODOMA**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMNISTRATION BY NOEL SAMWEL LIGOHA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 Of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 05 day of 07...................... 2024

Dated at Dodoma this 05 day of 06................2024

DISTRICT MAGISTRATE

RESIDENT MAGISTRATE I/C DODOMA DISTRICT

---

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701**

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701**

**OFISI ZA MATANGAZO Mikocheni Industrial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam.**
**Mob: +255 - 0677020701**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**Website: www.ippmedia.com**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Miili ya Wapalestina yakutwa kwenye kaburi moja Al Shifa

**GAZA,** Palestina

BAADA ya wanajeshi wa Israel kuondoka katika jengo la Hospitali ya Al-Shifa katika mji wa Gaza mwezi Aprili, kumegunduliwa miili ya watu waliozikwa katika makaburi ya pamoja.

Taarifa kutoka ndani ya jengo hilo, ilieleza Wapalestina waliokuwa wakitafuta mabaki ndani ya magofu ya hospitali hiyo iliyoteketezwa walisema walikuta miili ya watu iliyofukiwa pamoja katika eneo hilo.

Katika kipindi cha miezi minane ya vita, hospitali zimekuwa zikishambuliwa mara kwa mara, huku Israel ikidai kuwa zinatumiwa kama vituo na wanamgambo wa Hamas; kitu ambacho kundi hilo linakanusha.

Hata hivyo, Al-Shifa ambayo zamani ilikuwa kituo kikubwa cha matibabu na chenye vifaa bora zaidi katika Ukanda wa Gaza, imesababisha mshangao na hofu zaidi.

Uvamizi huo uliofanywa kwa kushtukiza wa wiki mbili zilizopita ulielezwa na Israel kama kuwadhibiti kuwa Hamas waliojipanga upya katika eneo hilo.

Msemaji wa serikali ya Israel, Avi Hyman, alisema waliwaondoa magaidi 200 na wengine 900 waliwakamata bila hata raia mmoja kujeruhiwa.

Ilielezwa ndani ya hospitali hiyo miili ya watu iliyooza ikitolewa katika tuta la mchanga iliyorundikwa na tingatinga katika ua wa hospitali hiyo.

Kutokana na hali hiyo, hata madai ya kwamba hakukuwa na raia waliojeruhiwa yalitiliwa shaka.

Katika wiki za hivi karibuni, makaburi manne ya halaiki yamegunduliwa katika eneo hilo, huku timu za watafutaji wa Palestina zikisema kuwa mamia ya maiti zimepatikana.

**BBC**

# Bunge la Marekani lapitisha vikwazo maofisa wa ICC

**WASHINGTON,** Marekani

BUNGE la Wawakilishi la Marekani, limepiga kura kupitisha sheria ambayo itaiwekea vikwazo Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu (ICC) baada ya mwendesha mashtaka wake kuomba hati ya kukamatwa kwa maofisa wa serikali ya Israel.

Wabunge hao wamechukua hatua hiyo baada ya mwendesha mashtaka wa mahakama hiyo yenye makao makuu yake mjini The Hague, nchini Uholanzi, kutaka Waziri Mkuu wa Israel Benjamin Netanyahu na Waziri wa Ulinzi wa Israel, Yoav Gallant wakamatwe kwa tuhuma zinazohusiana na vita vya Ukanda wa Gaza.

Mahakama hiyo pia anatafuta vibali vya kukamatwa kwa viongozi watatu wa kundi la Hamas.

Mswada huo uliopendekezwa na wabunge wa Chama cha Republican wanaounga mkono Israel, unalenga maofisa wa ICC waliohusika katika kesi hiyo kuwazuia kuingia Marekani.

**Wabunge hao wamechukua hatua hiyo baada ya mwendesha mashtaka wa mahakama hiyo yenye makao makuu yake mjini The Hague, nchini Uholanzi, kutaka Waziri Mkuu wa Israel Benjamin Netanyahu na Waziri wa Ulinzi wa Israel, Yoav Gallant wakamatwe kwa tuhuma zinazohusiana na vita vya Ukanda wa Gaza.**

Kura hiyo iliyopigwa Jumanne, ilipita kwa wingi wa uungwaji mkono wa kura 247 kati ya 155.

Warepublican wawili walipiga kura ya kupinga na wabunge 42 wa Democratic wanaounga mkono sheria hiyo.

Ingawa mswada huo ulipitishwa katika Bunge, hautarajiwi kuwa sheria.

Sheria hiyo huenda ikapuuzwa na wabunge wa Democratic wanaodhibiti Bunge la Seneti la Marekani na itabidi ipitishwe kabla ya kutiwa saini na rais kuwa sheria.

Lakini Rais Joe Biden alidokeza kuwa anapinga vikali mswada huo na utawala wake hauungi mkono vikwazo hivyo.

**BBC**



Wapalestina wakikusanyika ndani ya jengo la Hospitali ya Al Shifa kutafuta miili ya ndugu zao jana. **PICHA: REUTERS**

# Lissu: Msigwa anastahili kuigwa

**Na Christina Mwakangale**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, amesema Mchungaji Peter Msigwa anastahili pongezi kutokana na dhamira yake ya kujitolea kuhudumia wananchi.

Lissu alitoa kauli hiyo jana akiwa kwenye ziara Kijiji cha Ughandi, mkoani Singida alikomtambulisha Mchungaji Msigwa jukwaani, huku akimtaja "ni mgeni muhimu anayefaa kuigwa".

"Tumepata mgeni na kumsikiliza, nimpe shukrani Mchungaji Msigwa kwa kuja kunisikiliza. Hajalipiwa mafuta, hajalipiwa posho, amekuja kwa gharama zake.

"Ninamshukuru Mchungaji Msigwa kwa kutukumbusha na kutufundisha umuhimu wa kujitolea... kwa sababu hii kazi kubwa ya kuelimisha nchi inahitaji kujitolea," alisema Lissu.

Ulikuwa mkutano wa kwanza wa hadhara kwa Mchungaji Msigwa tangu ashindwe kutetea nafasi ya Mwenyekiti wa Kanda ya Nyasa ya CHADEMA na Joseph Mbilinyi 'Sugu' katika uchaguzi uliofanyika wiki iliyopita.

Mchungaji Msigwa aliibukia katika ziara hiyo ya Makamu Mwenyekiti Lissu siku mbili baada ya kutangaza kukata rufani kupinga kushindwa kwake na Sugu.

Katika mkutano wa jana wa Lissu, Mchungaji Msigwa alisema amefunga safari kutoka Iringa hadi Singida ili kufikisha ujumbe aliodai "muhimu kwa wananchi" wa mkoa huo wa Kanda ya Kati.

"Leo (jana) tumekuja kwenu, mbele yetu tuna Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Mchungaji Msigwa alisema, ni uchaguzi unaohusisha vitongoji vya vijiji, lakini bado tuko njiapanda... nchi yetu inahitaji Katiba Mpya.

Tukishamaliza uchaguzi huu, mwakani tuna Uchaguzi Mkuu, lakini kuna kitu kimoja wananchi hamwelewi. Nilitegemea hapa kijijini kwenu mambo yangekuwa mazuri.

Ninasema msiichague CCM (Chama Cha Mapinduzi), kwenye nafasi za uongozi kuanzia nafasi ya mwenyekiti wa kijiji, kitongoji hadi mtaa, wachagueni wagombea wa CHADEMA mlete mabadiliko."

Alisema Katiba Mpya itawapa wananchi mamlaka ya kusimamia mifumo ya kodi ambayo itazingatia tofauti za kipato cha mtu kulingana na chanzo chake cha uzalishaji.

"Mtuunge mkono kwenye harakati hizi, anayeteuliwa hana nguvu kuliko kiongozi anayechaguliwa na ninyi - wananchi, mbadilike!".

Lissu amekuwa na mikutano mkoani Singida tangu Jeshi la Polisi lilipomkabidhi gari lake lenye matundu yaliyotokana na shambulio la risasi la Septemba 7, 2017 jijini Dodoma.

# Makonda atumia waraka wa CAG kupekua kashfa kila halmashauri

**Na Beatrice Shayo**

BAADA ya ziara ya siku sita katika wilaya zote za mkoa, Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda, amesema zamu inayofuata ni kushughulikia hoja za ukaguzi zilizoainishwa katika ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika halmashauri zote za mkoa huo.

Makonda aliyasema hayo juzi katika mkutano wa hadhara uliofanyika katika Kata ya Mateves, Halmashauri ya Arusha wilayani Arumeru, mkoani Arusha.

"Tunatakiwa kukagua hesabu za ripoti ya CAG katika halmashauri zote kuangalia ripoti ya CAG inasema hapa mmepiga hela na kama wamepiga hela na mimi nawapiga spana," alisema Makonda.

Katika ripoti ya CAG kwa mwaka 2022/23 katika mamlaka za serikali za mitaa, kwenye halmashauri za mkoa wa Arusha yaliainishwa mambo kadhaa yakiwamo uchepushaji fedha kwenda miradi isiyopangiwa fedha hizo, usimamizi wa mikataba usiozingatia taratibu na mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na wenye ulemavu.

Pia kuna hoja kuhusu kodi za zuio katika halmashauri zisizowasilishwa Mamlaka ya Mapato Tanzania, Malipo Bohari ya Dawa (MSD) bila vifaa tiba kutolewa, usimamizi ununuzi wa mikataba bila kufuata taratibu, na vifaa tiba kupokewa bila kutumika. Makonda pia alisema watapita kila kata na anatuma salamu kwa watendaji wa kata kama kuna mambo ambayo hayajakaa vizuri, wajipange.

"Kama kuna mtendaji kuna mambo ambayo yamekaa ovyo, ayaweke vizuri na katika mikutano yetu asije kama mtalii vinginevyo utakuja na cheo utaondoka bila cheo wala mimi sina shida. Nitaenda kulala usingizi mzuri shida yangu ni wananchi wanaolia kuhusu haki zao wapate haki zao," alisema Makonda.

Alisema kuna tukio lingine la 'Karibu Fair' ambalo litahusisha kampuni takribani 800 na zaidi ya nchi 50 kwa siku tatu kwa ajili ya maonyesho ya biashara na tayari maandalizi yamefanyika katika eneo la Kisongo.

Makonda aliwakaribisha wananchi kujitokeza kwa wingi kwa ajili ya kujionea fursa mbalimbali zitakazoletwa na makampuni hiyo.

Aidha, Makonda alisema Juni 24, mwaka huu, watatoa huduma za matibabu bure kwa wananchi wa mkoa wa Arusha kwa siku saba.

"Tunawaleta madaktari bingwa kutoka hospitali kubwa Tanzania zikiwamo Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Taasisi ya Saratani ya Ocean Roads, Aga Khan na SAIFEE. Katika kambi hiyo, kama ni masuala ya figo yatapatiwa uchunguzi na ushauri na kila aina ya ugonjwa utapimwa. Ukibainika unaumwa utatibiwa bure," alisema Makonda.

# JKU SC YAWEKA MGUU MMOJA MICHUANO CAF

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

VINARA wa Ligi Kuu Zanzibar, JKU SC wamefanikiwa kutinga hatua ya fainali ya mashindano ya kuwania Kombe la Shirikisho la Soka visiwani humo (ZFF FA CUP), baada ya kuifunga Uhamiaji kutoka Kanda ya Unguja penalti 4-1.

JKU ililazimika kusubiri hadi hatua ya matuta baada ya timu hizo kushindwa kufungana katika dakika 90 za kawaida.

Baada ya matokeo hayo, sasa JKU inasubiri mshindi kati ya mechi itakayochezwa kesho kati ya Hard Rock dhidi ya Chipukizi kutoka Kanda ya Pemba.

**Akizungumza na gazeti hili jana huku akiwa na furaha, Kocha Mkuu wa JKU, Salum Ali, alisema kwa hatua ambayo wamefika tayari kikosi chake kimepata mafanikio.**

Ali alisema mpaka anaamini kikosi chake kina asilimia kubwa ya kupata ushindi katika mechi ya fainali ya michuano hiyo ya msimu huu na pia wakiwa kwenye mbio za kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar.

„Mchezo wao dhidi ya Uhamiaji ulikuwa mgumu kwa sababu wapinzani wao pia walihitaji ushindi ili kupata nafasi ya kuvuka hatua hiyo, nawapongeza sana wachezaji wangu kwa kupambana,“ alisema Ali.

Aliongeza wapinzani wao walikuja na mbinu ya kusaka magoli ya mapema ili kujiweka katika mazingira ya kusonga mbele lakini hakuna upande uliofanikiwa kupata bao katika dakika za kawaida za mechi hiyo.

"Ulikuwa ni mchezo wenye ushindani mkubwa, katika dakika zote 90, kosa kosa na mashambulizi yalizua presha sio tu katika benchi letu, lakini hata kwa wapinzani wetu, kama tujuavyo hatua ya penati inakuwa ni bahati hivyo bahati ilituangukia sisi,"Ali alisema.

Aliongeza wataendelea kujiimarisha ili kuhakikisha hawapotezi mchezo wa fainali na hatimaye kubeba kombe la mashindano hayo msimu huu.



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha (mwenye miwani), akiwaaga wanafunzi wanaokwenda kushiriki Mashindano ya Umoja wa Michezo na Taaluma kwa Wanafunzi wa Shule za Msingi (UMITASHUMTA), yatakayofanyika Tabora mwaka huu. Shinyanga ilimaliza katika nafasi ya tatu kwenye michuano hiyo mwaka jana. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Frank atamba kumchapa Komando

**Na Shufaa Lyimo**

BONDIA wa ngumi za kulipwa nchini, Frank Sebastian, amesema hana hofu yoyote ya kukutana na mpinzani wake Barnaba Alexander ‚Komando Muuza Madafu‘ kuelekea katika pambano la Dar Boxing Derby litakalofanyika Juni 29, mwaka huu kwenye viwanja vya Kijitonyama, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Sebastian alisema yupo tayari kwa ajili ya pambano hilo na ametamba mpinzani wake hana uwezo wa kumchapa watakapokutana na badala yake amemtaka aendelee biashara yake ya kuuza madafu.

Bondia huyo alisema amefanya mazoezi kwa muda mrefu ili kuhakikisha anafanya vyema katika pambano hilo na amejipanga kumaliza ‚kazi‘ mapema.

"Ninaendelea kufanya mazoezi ili kuuweka imara mwili wangu, ninaamini siku hiyo nitatoa burudani kwa kuhakikisha ninamtwanga ‚Muuza Madafu‘ ataka afahamu mimi ni nani, " alitamba Frank.

Aliongeza anaamini yeye ana uwezo mkubwa ukilinganisha na mpinzani wake na anachosubiri ni muda wa pambano ufike.

"Natangaza vita kwa sababu sitamwonea huruma siku hiyo, nimejiandaa kumpasua, atarajie kupokea kipigo ambacho hatakisahau katika maisha yake yote," bondia huyo alisema.

Amewaomba mashabiki wake wajitokeze kwa wingi siku ya pambano hilo kushuhudia atakavyomchapa mpinzani huyo mpya kwenye mchezo wa ngumi.

## Kikapu U-18 kamili kuchuana Uganda

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya Taifa ya Kikapu ya vijana wenye umri chini ya miaka 18 inatarajiwa kuelekea Uganda kwa ajili ya kushiriki mashindano ya kuwania kufuzu michuano ya Afrika kwa vijana itakayofanyika kuanzia Juni 9 hadi 14, mwaka huu nchini humo.

Ofisa Habari wa Shirikisho la Mpira wa Kikapu Tanzania (TBF), Mary Arthur, aliliambia gazeti hili maandalizi ya safari hiyo yako katika hatua za mwisho na kila mchezaji morali yake ipo juu kuhakikisha wanapeperusha vizuri bendera ya taifa katika michuano hiyo.

„Maandalizi yanaendelea vyema na wachezaji wametumia muda mrefu kufanya mazoezi ili kuimarisha viwango vyao kwa sababu wanakwenda Uganda kusaka ushindi na si kushiriki, „ alisema Arthur.

Aliongeza katika kujiweka sawa, timu hiyo jana jioni ilitarajiwa kucheza mechi ya kirafiki dhidi ya Oratory kwa upande wa wavulana na wanaamini mchezo huo utawasaidia wachezaji kupandisha viwango vyao.

„Lengo la kucheza mchezo huo ni kumpa nafasi kocha kuangalia mapungufu na kuyarekebisha, pia kuona uwezo wa wachezaji wake kabla hawajaanza safari, tunaomba Watanzania na wadau wetu waendelee kuiunga mkono timu hii ili tukatimize malengo tuliyojiwekea, „ aliongeza ofisa huyo.

## Riadha Zanzibar yatangaza kamati

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KATIKA kuhakikisha riadha itafanya vizuri, Shirikisho la Mchezo huo Zanzibar (ZAF), limeunda kamati tatu za kusimamia shughuli za maendeleo mbalimbali visiwani humo, imefahamika.

Rais wa ZAF, Muhidini Yasin, aliliambia gazeti hili wamefanya uamuzi huo kwa kufuata maelekezo ya katiba ya shirikisho hilo na kuzitaja kamati hizo ni Kamati ya Fedha na Mipango, Kamati ya Ufundi na Kamati ya Makocha.

Aliwataja wajumbe wanaounda Kamati ya Ufundi ni Kassim Hussein ambaye atakuwa Mwenyekiti, Makame Juma Hassan (Katibu) na wajumbe ni Fatuma Khamis, Omar, Hamad Kibano, Masoud Tawakal na Maulid Bakari Sharif.

Kamati ya Fedha na Mipango inautwa na Makame Ali Machano (mwenyekiti), Seif Khamis Mbarouk (katibu) na wajumbe ni Yussuf Risawali, Abdallah Amour Duchi, Salma Ali Suleiman, Abdul-Wahabi Dau Haji, Wanu Hafidh Ameir na Machano Ali Makame.

Aliwataja wanaounda Kamati ya Makocha ni Masoud Tawakal (mwenyekiti), Makame Haji Makame 'Tall' (katibu) na wajumbe ni Ali Issa Ali, Mohammed Abdi Shoka, Abdallah Issa Ramadhan, Sarah Othman, Fatuma Ahmed, Khamis Mohammed Ali, Maulid Nassor Maulid na Mohammed Suleiman Haji.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### TSYGANKOV ANUKIA ARSENAL
ARSENAL inamtazama winga wa Girona mwenye umri wa miaka 26 kutoka Ukraine, Viktor Tsygankov, ambaye anasakwa na AC Milan. (***Sport***)

### CHELSEA, ARSENAL VITANI
CHELSEA ina imani inaweza kushindana na Arsenal katika harakati za kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Slovenia, Benjamin Sesko, kutoka RB Leipzig ambaye ana umri wa miaka 21. (***Standard***)

### BRANTHWAITE AKARIBIA UNITED
MANCHESTER United imeonyesha nia ya kumsajili beki wa Everton na England, Jarrad Branthwaite, mwenye umri wa miaka 21, huku wakitafuta kuimarisha safu yao ya ulinzi. Beki wa Juventus na Brazil, Gleison Bremer (27), na mlinzi wa Nice na Ufaransa Jean-Clair Todibo (24), pia wanalengwa. (***Football Insider***)

### SANCHO, UNITED KITAELEWEKA
MANCHESTER United ipo tayari kufanya mazungumzo na winga wa England, Jadon Sancho, mwenye umri wa miaka 24, kabla ya kuamua kuhusu mustakabali wake. Sancho aliisaidia Borussia Dortmund kutinga fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya kujiunga nayo kwa mkopo kufuatia kutofautiana na Kocha Erik ten Hag. (***ESPN***)

### GARCIA ATAJWA LEVERKUSEN
KLABU ya West Ham inajaribu kuzuia jaribio la Bayer Leverkusen kumsajili kiungo wa kati wa Girona na Timu ya Taifa ya Hispania, Aleix Garcia mwenye umri wa miaka 26. (***Guardian***).

### WEST HAM YAMTAKA SILVA
WEST Ham pia wanataka kumsajili winga wa Vitoria Guimaraes na Timu ya Taifa ya Ureno, Jota Silva, mwenye umri wa miaka 24. (***Teamtalk***)

### SPENCE ATAKIWA SPURS
KLABU ya Tottenham Hotspur inamwania, Djed Spence, mwenye umri wa miaka 23, akitokea Genoa kwa mkataba wa kudumu baada ya beki huyo wa Uingereza kuonyesha kiwango kizuri akiwa katika klabu hiyo ya Italia. (***Fabrizio Romano***)

### PARDEW AITAKA NEWCASTLE
KOCHA wa zamani wa Newcastle United na West Ham, Alan Pardew, mwenye umri wa miaka 62, anasema amevutiwa na kazi ya kuinoa Burnley. (***Talksport***)

### ADARABIOYO SAFI CHELSEA
MLINZI wa Fulham, Tosin Adarabioyo, mwenye umri wa miaka 26, amefanyiwa uchunguzi wa kimatibabu kabla ya kuhamia rasmi Chelsea. (***Mail***)

### DYBALA KUHAMIA ENGLAND
MSHAMBULIAJI wa AS Roma mwenye umri wa miaka 30, Paulo Dybala, yuko tayari kuhamia Ligi Kuu England katika msimu mpya wa mashindano. (***Sky Sports***)

### LAMPARD ATAJWA BIRMINGHAM
KLABU ya Birmingham City imefanya mazungumzo na kocha wa zamani wa Chelsea na Everton, Frank Lampard. Kocha huyo pia yuko katika rada za Burnley baada ya kuondoka kwa Vincent Kompany aliyejiunga na Bayern Munich. (***Football Insider***)

### SOLSKJAER KUTUA BESIKTAS
KOCHA wa zamani wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, mwenye umri wa miaka 51 anasakwa na Besiktas ya Uturuki. Solskjaer hajafanikiwa kupata kazi tangu alipoondoka United Novemba mwaka, 2021. (***Mirror***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# FERNANDES ANATAKA MSHAHARA MKUBWA

**MANCHESTER,** England

## Lakini asema hatima yake itatokana na bosi atakayeinoa United...

BRUNO Fernandes anatafuta nyongeza ya mshahara na kuhakikishiwa nafasi yake kuhusu mpango wa muda mrefu wa Manchester United anapofikiria kuondoka katika klabu hiyo msimu huu wa joto, ripoti imedai.

Mustakabali wa Fernandes Old Trafford uliwekwa shakani mapema msimu huu wa joto kufuatia ripoti za uwezekano wa kufanyiwa marekebisho ya kikosi, ambapo kiungo huyo alikiri anaweza kufikiria hatima yake iwapo hajisikii kuthaminiwa tena chini ya mmiliki mwenza mpya, Sir Jim Ratcliffe na INEOS.

Baada ya kuzua uvumi huo, Fernandes alianza kutuliza hofu kwa kukiri mapenzi yake kwa United, ingawa hiyo ilifuatiwa na ripoti ya wakala wake alikuwa na mazungumzo na timu mbalimbali za Ulaya.

Sasa, gazeti la The Guardian limeandika, Fernandes anatafuta kujitolea zaidi kutoka kwa United ikiwa anataka kuahidi mustakabali wake kwa Mashetani Wekundu.

**Fernandes anasemekana kudai nyongeza ya mshahara kwa kiwango ambacho kitamfanya kuwa karibu na wachezaji wanaolipwa fedha nyingi zaidi klabuni hapo.**

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno anapokea kitita cha pauni 220,000 kwa wiki lakini anaamini anastahili kuwa karibu zaidi na mchezaji anayelipwa kiasi cha pauni 365,000, Marcus Rashford.

Pia katika mawazo ya Fernandes ni mpango wa muda mrefu wa klabu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 kwa muda mrefu amekwa wazi anataka kuona matarajio yake yakilinganishwa na wale wanaoongoza.

Mengi yanaweza kutegemea mustakabali wa Kocha Erik ten Hag, ambaye kuendelea kwake Old Trafford kutaamuliwa hivi karibuni na Ratcliffe.

Iwapo Ten Hag ataondoka, Fernandes anataka kujua ni nani atachukua nafasi ya Mholanzi huyo kabla ya kuamua kama atataka kuondoka majira ya kiangazi.

United haiaminiki inajaribu kumuuza Fernandes, lakini kuna ufahamu yeye ni mmoja wa mali ya thamani zaidi katika klabu hiyo na fedha zitakazopatikana kutokana na kuondoka kwake zitasaidia sana kusaidia kukijenga upya kikosi chao.

HABARI MICHEZO

# LAPORTA AFUNGUKA KILICHOMTESA XAVI



**BARCELONA,** Hispania

RAIS wa Barcelona, Juan Laporta, amefichua mashaka kuhusu Xavi Hernández kutokiamini kikosi cha sasa yalisababisha uamuzi wa kumbadilisha na Kocha mpya, Mjerumani Hansi Flick mwezi uliopita.

Akizungumza kwa mara ya kwanza tangu kumtimua Xavi, Laporta pia alithibitisha nia ya Barca kuongeza mkataba wa mkopo wa João Félix na João Cancelo na kusajili kiungo na winga, huku akisisitiza hali ya kifedha ya klabu hiyo haitawalazimu kusikiliza ofa kwa wachezaji wao bora majira ya joto.

Awali Xavi alikuwa ametangaza Januari angejiuzulu mwishoni mwa msimu, na kubatilisha uamuzi wake ilipofika Aprili, mwaka huu.

Hata hivyo, wiki tatu tu baadaye, Laporta alimfukuza.

"Ikiwa Xavi anaweza kubadilisha mawazo yake, sisi pia tunaweza," alisema Laporta katika mahojiano na Barca One, chaneli ya televisheni ya ndani ya klabu hiyo ya Katalunya.

"Kila kitu kililazimishwa kidogo tulipoamua kumbakisha. Xavi ni gwiji wa klabu na shauku yake ilitufanya tufikie uamuzi wa kuidhinisha nafasi yake.

"Wakati wa zamu yake, nilimuuliza: 'Je, unaamini katika timu?' Aliniambia 'Ndiyo.' Alisema ana imani na timu hii.

"Lakini wakati huo kulikuwa na maoni ambayo alibadilisha mazungumzo yake na Mkurugenzi wa Michezo, Deco kuhusiana na mabadiliko muhimu katika kikosi.

"Hilo lilinilazimu kufikiria upya hali hiyo na nilihisi kikosi kinahitaji msukumo mpya ili kuwa na ushindani zaidi na kupata kilicho bora zaidi ya kile tulichonacho.

"Nimelazimika kufanya maamuzi haya magumu na magwiji wa Barca. Moyo wangu uliniambia nifanye jambo.

"Natumaini uhusiano wetu unaweza kuendelea. Nimeupitia kwa Ronald Koeman, Lionel Messi, Gerard Piqué, Sergio Busquets, Jordi Alba na sasa Xavi. Maamuzi yote yanafanywa kwa ajili ya nia nzuri kwa Barca -- klabu inakuja kwanza."

Kinyume chake, Laporta alisema Flick anahisi Barca, ambao walimaliza katika nafasi ya pili katika LaLiga na kutoka kwenye Ligi ya Mabingwa katika hatua ya robo fainali 2023-24, wanaweza kufanikiwa wakiwa na timu ya sasa.

"Flick anahisi uwezo wa kushindana na kikosi hiki," rais huyo alieleza.

Laporta alisema moja ya kazi ya Flick itakuwa kuboresha utimamu wa wachezaji, akibainisha ni eneo ambalo walitatizika chini ya Xavi.

"Kazi ya Flick ni kushinda na amekubali changamoto," aliendelea.

"Wachezaji lazima wajitayarishe vyema kimwili. Vijana, wachezaji wa akiba, wachezaji kama Robert Lewandowski ... kila mmoja lazima awe katika hali nzuri kimwili.

"Maandalizi ya kimwili ni muhimu kwa sababu, tunaweza kushinda kila kitu. Msimu huu tuliona timu ikicheza kimwili baada ya dakika ya 60. Hatukumaliza michezo kama tulivyotaka, katika Clásicos mbili, kwa mfano.

"Sisemi timu haikujiandaa vyema, lakini daima kuna mambo ya kuboresha. Tunahitaji zaidi."

## Kuna watu walininyima furaha PSG - Mbappé

**PARIS,** Ufaransa

KYLIAN Mbappé amesema baadhi ya watu ndani ya Paris Saint-Germain walimkosesha furaha katika mkutano wake wa kwanza na waandishi wa habari tangu akamilishe uhamisho wa kutua Real Madrid.

Mbappé alijiunga rasmi na Madrid kwa uhamisho wa bure mapema wiki hii na kumaliza sakata hilo la muda mrefu.




"Sikuwa na furaha PSG," alisema Mbappé katika mkutano na waandishi wa habari akiwa na Timu ya Taifa ya Ufaransa Jumanne.

"Kuna mambo fulani yalinikosesha furaha, lakini mchezaji kama mimi sikuweza kuonyesha hivyo kwa sababu mimi ni kiongozi, hivyo nilijaribu kuwa chanya kadri niwezavyo.

Kocha, wachezaji na wafanyakazi wa klabu waliniunga mkono, na itakuwa mbaya kuja na kusema sikuwa na furaha lakini mambo fulani na watu walinikosesha furaha."

Mbappé alihusika katika mzozo msimu uliopita wa kiangazi na Rais wa PSG, Nasser Al-Khelaifi, kuhusu iwapo angeongeza mkataba wake au la hadi mwisho wa msimu huu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 aliongeza kuwa klabu ya Paris ilimwambia hatacheza kabisa katika msimu ambao umekamilika, lakini kocha wa timu hiyo, Luis Enrique na Mkurugenzi wa Michezo, Luis Campos, walimwokoa.

Mbappé alisema: "Walinifanya nielewe sitacheza, waliniambia usoni mwangu, waliniambia kwa ukali.

"Luis Enrique na Luis Campos waliniokoa. Nisingekanyaga tena uwanjani bila wao."

## Fedha kumpeleka De Bruyne Saudia

**MANCHESTER,** England

KELVIN De Bruyne amesema yuko "wazi" kuhamia Ligi Kuu ya Saudia Arabia kutokana na faida „ya ajabu" ya kifedha.

Kiungo huyo wa kati wa Manchester City amebakiza mwaka mmoja katika mkataba wake pale Etihad na amekuwa akihusishwa na kuhamia Saudi Arabia.

Chanzo kimoja kiliambia ESPN wawakilishi wa De Bruyne walitembelea klabu 10 za Saudia ndani ya siku tatu ndani ya Mei na mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji amekiri anavutiwa na motisha ya fedha nchini humo.

„Katika umri wangu lazima uwe wazi kwa kila kitu," alisema De Bruyne katika mahojiano na kituo cha Ubelgiji cha HLN.

"Unazungumza juu ya kiasi cha ajabu cha fedha katika kile ambacho kinaweza kuwa mwisho wa kazi yangu. Wakati mwingine unapaswa kufikiria juu ya hilo.

„Ikiwa nitacheza huko kwa miaka miwili, nitaweza kupata kiasi cha ajabu cha fedha. Kabla ya hapo ningelazimika kucheza mpira wa miguu kwa miaka 15. Huenda nisifikie kiasi hicho bado.

"Basi inabidi ufikirie kuhusu hilo linaweza kumaanisha nini baadaye. Lakini kwa sasa sijalazimika kufikiria hilo bado."

De Bruyne amekaa kwa miaka tisa City, akishinda taji la Ligi Kuu England mara sita.

Alicheza mechi 18 za ligi msimu uliopita baada ya kukosa miezi mitano ya kwanza ya kampeni kwa sababu ya jeraha la misuli ya paja.

Sasa De Bruyne mwenye umri wa miaka 32, ambaye amehusishwa na kuhamia Marekani (MLS), alisema ni wakati wa kuanza kufikiria juu ya uhamisho wake ujao.

"Haya ni mazungumzo ambayo tunazidi kuwa nayo kama familia," aliongeza De Bruyne.

"Bado nina mwaka mmoja katika mkataba wangu, hivyo ni lazima nifikirie nini kinaweza kutokea, mwanangu mkubwa kwa sasa ana umri wa miaka nane na hajui lolote ila England.

"Pia anauliza nitaichezea City kwa muda gani. Muda ukifika, tutalazimika kukabiliana nayo kwa njia fulani."



HABARI MICHEZO

# Simba na kikao 'kizito'

INATOKA UK. 24

yatapelekea kuwa na kikosi kipana na timu ‚iliyobalansi,“ aliongeza.

Pia kikao hicho kinatarajia kupendekeza mahali ambayo kikosi chao kitaenda kuweka kambi.

„Usajili utafanyika kwa nafasi nyingi, safu ya ulinzi itaongezewa watu, kiungo na ushambuliaji pia, Simba ya msimu ujao itakuwa ya tofauti sana, kwa kifupi tunataka kudumisha umoja wetu ambao utasaidia kufikia malengo, viongozi wakiwa pamoja hakuna tutakapofeli,“ alisema mtoa habari huyo.

Naye Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema kila kitu kinachofanywa na klabu hiyo kitawekwa hadharani ili mashabiki na wanachama watafahamu muda wake sahihi utakapofika.

„Kwa sasa sina la kusema, lakini muda ukifika kila kitu kitafahamika, tunafahamu Wana-Simba wanashauku ya kujua nini kitafanyika,“ alisema Ahmed.

Mbali na Ligi Kuu Tanzania Bara, Kombe la Fa, Simba itajiandaa kushiriki mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika baada ya kumaliza msimu uliopita katika nafasi ya tatu nyuma ya mabingwa Yanga na Azam FC.



# MATAMPI AANZA KUTIKISA USAJILI WA COASTAL UNION

**Na Faustine Feliciane**

GOLIKIPA wa Coastal Union, Ley Matampi, amesema kwa sasa yupo tayari kujiunga na timu yoyote itakayomhitaji baada ya kumaliza mkataba wake wa kutumikia klabu hiyo ya jijini, Tanga.

Matampi amesema hayo kufuatiwa kauli iliyotolewa kuwa bado ana mkataba na Coastal Union ambayo ameisaidia kumaliza msimu uliopita katika nafasi ya nne na kukata tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

**Kipa huyo ambaye anatajwa kutakiwa na baadhi za hapa nchini ikiwamo Simba, amesema amesha maliza mkataba wake na Coastal Union na sasa yuko huru kufanya mazungumzo na timu nyingine.**

„Timu yoyote inayonihitaji nipo tayari kufanya mazungumzo, mkataba wangu umeisha, unajua nilisaini mkataba wa mwaka mmoja tu, hayo mengine mimi siyajui,“ alisema Matampi.

Aliongeza hata kama atabaki katika klabu hiyo, itawalazimu waanze mazungumzo mapya na wakikubaliana ataridhia kusaini mkataba mpya.

Hivi karibuni Simba imetajwa kutaka huduma ya golikipa huyo raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), kwa ajili ya kuimarisha kikosi chake wakati pia wakijipanga kumbakisha Mwarabu wa Morocco, Ayoub Lakred.

Matampi ameonyesha uwezo mkubwa msimu huu kwa kucheza michezo 15 bila kuruhusu goli akimfunika Djigui Diarra wa mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga.

Katibu Mkuu wa Coastal Union, Omar Ayoub, amekaririwa juzi akisema golikipa huyo bado ana mkataba wa mwaka na timu hiyo na klabu yoyote inayomhitaji inapaswa kuwasiliana na uongozi wa mabingwa hao wa mwaka 1988 ili kufanya ‚biashara‘.



Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi (wa pili kulia), akiwa na wasaidizi wake wakifurahi baada ya kutwaa Kombe la FA katika fainali iliyochezwa kwenye Uwanja wa New Amaan Complex, Zanzibar Jumapili iliyopita. **PICHA: MTANDAO**

# Chalenji Cup kuanza Juni 29

**Na Somoe Ng'itu**

MASHINDANO ya Kombe la Chalenji kwa nchi za Afrika Mashariki na Kati yamepangwa kufanyika kuanzia Juni 29 hadi Julai 14, mwaka huu jijini, visiwani Zanzibar imefahamika.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Baraza la Soka Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), Auka Gecheo, aliliambia Nipashe kuwa maandalizi kuelekea mashindano yanaendelea vyema na wanaamini timu zote wanachama zitashiriki.

Gecheo alisema pia kutakuwa na timu waalikwa kwa lengo la kuongeza ushindani katika michuano hiyo, lakini itawasaidia kujiandaa na mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN).

„Baada ya kufanyika kwa mafanikio Mashindano ya Shule ya Afrika huko Zanzibar, sasa tunajiandaa kuendesha michuano ya Kombe la Chalenji, tunatarajia wachezaji wataonyesha ushindani na viwango vya juu katika michezo yote,“ Gecheo alisema.

Mara ya mwisho CECAFA kuandaa mashindano hayo ilikuwa mwaka 2019 na wenyeji Uganda walitwaa ubingwa baada ya kuifunga Eritrea katika fainali zilizofanyika jijini, Kampala.

CECAFA pia imetangaza kurejesha mashindano ya Kombe la Kagame yatayofanyika kuanzia Julai 20 hadi Agosti 4, mwaka huu jijini, Dar es Salaam.

# SportPesa yaipa Yanga mamilioni

INATOKA UK. 24

ambayo kimkataba kwa sisi kushinda Ligi Kuu, Kombe la FA na kufika hatua ya robo fainali ya mashindano ya Ligi ya Mabigwa Afrika.

Huu ni msimu wa tatu mfululizo tumekuwa tukichukua ubingwa na kupata bonus hizi kutoka SportPesa. Tulianza na kuingia robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika, baada ya hapo tumechukua taji la Ligi Kuu na mwisho tumechukua Kombe la FA, na leo (jana), hii tunawakabidhi makombe yote kama wadhamini wakuu".

Rais huyo aliahidi Yanga itaendelea kujiimarisha ili kufanya vizuri zaidi katika msimu mpya wa mashindano.


„Tunawaahidi tutaendela kujenga timu imara ya ushindani ndani na nje ya Tanzania ili kuitangaza zaidi SportPesa ambaye ndiye mdhamini wetu mkuu," alisema Hersi.

Aliongeza wamewapa mapumziko wachezaji wao na wanatarajia kuanza kambi rasmi kwa ajili ya msimu mpya mapema mwezi ujao.

SportPesa imetimiza miaka saba tangu kuanzishwa kwake pamoja na kuidhamini Yanga.

Michezo
Alhamisi Juni 6, 2024
Nipashe

UK. 21



## Fernandes anataka mshahara mkubwa



Wachezaji wa Timu ya Taifa ya England wakifanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya kirafiki dhidi ya wenzao wa Iceland itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Wembley. England inajiandaa na michuano ya EURO 2024 itakayofanyika Ujerumani. **PICHA: MTANDAO**

## Simba na kikao 'kizito'

**Na Faustine Feliciane**

UONGOZI wa Simba ya jijini Dar es Salaam umeanza vikao vya kufanya uamuzi kwa ajili ya kujenga kikosi imara kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano mbalimbali watakayoshiriki, imefahamika.

Taarifa zilizopatikana kutoka ndani ya timu hiyo zimesema kikao hicho kitaanza na mchakato wa kuwaacha wachezaji ambao haiwahitaji kuelekea msimu ujao na kuwapa mikataba wote ambao wako kwenye mipango yao.

„Tutakuwa na kikao ‚kizito' kwa ajili ya kuhakikisha mikakati ya usajili inakwenda vizuri, tunatarajia kufanya usajili wa kishindo utakaorudisha timu yetu kwenye makali yake," kilisema chanzo chetu.

Kiliongeza kuwa viongozi wa timu hiyo wameamua kuunganisha nguvu na ili kuhakikisha wanakamilisha vyema mipango ya usajili na programu ya mazoezi na mambo yote muhimu kwa ajili ya msimu ujao.

„Hata suala la usajili linajadiliwa kwa pamoja, tayari kuna mambo mengi mazuri yapo katika hatua ya utekelezaji, mashabiki na wanachama wa Simba wasubiri kuona mabadiliko katika timu," kiliongeza chanzo hicho.

Taarifa zaidi ziliongeza tayari ipo orodha ya wachezaji wanaowawinda na kilichobakia ni uamuzi wa mwisho ambao utafanyika kwa kufuata mapendekezo yaliyotolewa na benchi la ufundi.

„Wapo wachezaji ambao ki ukweli wamepoteza sifa ya kuendelea kuwa katika kikosi cha Simba, matokeo ambayo tumeyapata msimu huu yametuumiza sana, tunataka kujenga kikosi kipya, imara ambayo kitarudisha heshima yetu.

Simba itafanya maboresho ya kikosi katika maeneo mengi ambayo

INAENDELEA UK. 23

# SportPesa yaipa Yanga mamilioni

## ●●● Ni baada ya kutwaa taji la Ligi Kuu, FA na kucheza robo fainali...

**Na Mwandishi Wetu**

MABINGWA wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga wamepokea hundi ya mfano ya Sh. milioni 537.5 kutoka Kampuni ya Burudani na Michezo ya Kubashiri SportPesa baada ya kufanya vizuri katika msimu uliomalizika wa 2023/24.

Makabidhiano hayo yamefanyika jijini Dar es Salaam jana, ikiwa ni siku chake zimepita baada ya msimu wa mashindano kumalizika hapa nchini.

Akizungumza jijini jana, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano cha SportPesa, Sabrina Msuya, aliwapongeza Yanga kwa kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu, Kombe la FA na kucheza hatua ya robo fainali ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Msuya alisema hayo ni mafanikio mazuri na hiyo imetokana na juhudi mbalimbali walizofanya katika msimu huu na hatimaye kushinda mataji hayo.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi SportPesa, Tarimba Abbas, naye aliwapongeza wachezaji, benchi la ufundi na viongozi wa Yanga kwa kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara mara tatu mfululizo.

"SportPesa siku zote imekuwa ikijivunia mahusiano ya kiudhamini kati ya kampuni na Young Africans na hapajawahi kutokea muda tukajutia kwa sababu tumejihusisha na klabu ambayo inaendeshwa kiweledi. Kwanza kabisa tungependa kupongeza uongozi ulioko chini ya Rais, Hersi Said, uongozi ambao umejenga timu ambayo ni imara, aina ya wachezaji ambao inawasajili, benchi la ufundi kiasi Yanga imekuwa ni timu inayojitosheleza kwa ushindani wa aina yake katika bara la Afrika.

**Ni jambo ambalo Sport Pesa tunaona tumefikia malengo yetu. Kila tuna chokiahidi kimkataba tumekitekeleza bila kuchelewa na Yanga ina hitaji mdhamini wa sam puli kama SportPesa. Leo tumekabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni 537.5," alisema Tarimba.**

Aliwaomba Yanga kutobweteka na mafanikio hayo na badala yake kuboresha timu yao kwa sababu anaamini msimu wa mwaka 2024/25 utakuwa na ushindani zaidi.

Kwa upande wake, Hersi aliwashukuru wadhamini hao kwa namna ambavyo wameshirikiana na Yanga kama mdhamini mkuu katika kutekeleza mipango na majukumu ya kila siku.

"Nichukue nafasi hii kuishukuru SportPesa kwa kutekeleza kwa wakati makubaliano yaliyopo kwenye mkataba kwa kutoa bonus ya Sh. milioni 537.5 baada ya klabu yetu kutwaa ubingwa huu wa Ligi Kuu Tanzania Bara na Kombe la FA.

Sisi kama Young Africans tumefurahi sana kupokea rasmi zawadi hii ya bonasi

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >